# Nipashe

Jumatano Oktoba 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580375

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



**FURSA**

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba : +255716500500
Barua Pepe: circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020


**WATIWA** mbaroni madai kumchoma moto mama

UKURASA 16



**MKE** wa Dk. Salim Ahmed Salim afariki dunia

UKURASA 3

# NEC: Ruksa kupiga tena kura ikikosewa

UKURASA 2

## Maalim Seif amtaka Membe kutochanganya wanachama

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Taifa, Maalim Seif Sharif Hamad, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu msimamo wake wa kumuunga mkono mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM awataka Watanzania kujiepusha chuki, ubaguzi

UKURASA 3




## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**SIRI WAGOMBEA CCM KUTOENGULIWA YAFICHULIWA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimefichua siri kuhusu wagombea wake kutoenguliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)...

UKURASA WA 4

**TAKUKURU YAREJESHA MAMILIONI YA WASTAAFU**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, imewarejeshea...

UKURASA WA 5

**MATUKIO MOTO SHULENI YAMWIBUA CAG ASSAD**

MFULULIZO wa matukio ya kuungua moto shule za Kiislamu katika...


**MICHEZO** SIMBA, YANGA SASA KUSUBIRI KWA AZAM UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# NEC: Ruksa kupiga tena kura ikikosewa

**Na Mwandishi Wetu**

MPIGAKURA anaruhusiwa kubatilisha uamuzi wake wa kura kituoni kwa kupiga nyingine ikiwa tu karatasi ya awali aliyotumia, hajaiingiza katika sanduku la kupigia kura.

Ofisa Utumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Flora Mkama, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari yaliyoandaliwa na tume kuelekea uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Jumatano ijayo.

Akiwasilisha mada kuhusu taratibu za upigaji kura, ufungaji wa vituturi na masanduku ya kura, Mkama alisema mpigakura kabla hajaiingiza kura yake kwenye sanduku la kura, anaweza kubatilisha uamuzi wake huo na kupiga kura upya.

"Anaweza kubatilisha uamuzi wake kwa kukabidhi karatasi ya awali kwa msimamizi ambaye ataiweka kwenye bahasha maalum na kuhesabika kama kura iliyoharibika na atapewa karatasi nyingine ili kupiga kura yake," alisema.

Ofisa Sheria NEC, Athumani Kimia, akizungumzia majukumu baada ya kupiga kura, alisema msimamizi wa kituo atatakiwa kuziweka karatasi za kura ambazo hazikutumika, zilizoharibika na sehemu ya kitabu cha karatasi ambazo hazikutumika ndani ya bahasha namba tatu 3.

"Bahasha namba 3A kwa uchaguzi wa Rais, bahasha namba 3B kwa uchaguzi wa wabunge na bahasha namba 3C kwa uchaguzi wa udiwani zinahusika katika hili," alisema.

Ofisa huyo alisema kura hizo ambazo zinahesabika kama zimeharibika, huwekwa kwenye bahasha namba 6A.

Akifafanua zaidi kuhusu mpigakura kubatilisha kura yake, Kimia alisema lengo ni kupata kura halali.

"Katika mazingira hayo, mpigakura ana haki ya kupewa karatasi nyingine, lakini sheria haijaweka ukomo wa utoaji wa karatasi, ila haiwezekani mtu apewe karatasi ya kwanza, ya pili mpaka nne uendelee kuharibu.

"Ikionekana uharibifu ni endelevu, basi mtu huyo atakuwa na matatizo, hivyo msimamizi atachukua uamuzi wa kumnyima," alifafanua.

Alisema ndiyo maana imeelezwa mpigakura ambaye hawezi kupiga kura mwenyewe, ana haki ya kwenda na mtu anayemwamini.

Kuhusu kura zenye mgogoro, Kimia alisema msimamizi anatakiwa kuzitatua kabla ya kutangaza matokeo ili kutoleta upungufu au kuongeza kura.

Akijibu swali kuhusu muda uliotengwa kwa ajili ya kusafirisha sanduku la mpigakura, Kimia alisema hakuna muda kamili ila itategemea mazingira.

Uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani umepangwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu, ikiwa ni mara ya kwanza kufanyika siku ya kazi. Tayari serikali imesema siku hiyo itakuwa ya mapumziko ili wananchi wapate haki ya kuchagua viongozi wanaowataka.



Mgombea urais kupitia CCM, Dk. John Magufuli akizungumza na wananchi katika mkutano wa kampeni kwenye viwanja vya Chuo cha Ualimu Korogwe, mkoani Tanga jana. **PICHA: IKULU**

# Maalim Seif amtaka Membe kutowachanganya wanachama

**Na Frank Maxmillian, TUDARCo**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amemtaka mgombea urais wa chama hicho, Bernard Membe, kutowachanganya wanachama wao kuhusu watakayempigia kura kwa nafasi ya urais.

Amesema viongozi wa chama hicho katika moja ya vikao vyao, walikubaliana wanachama wampigie kura mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, na kwa Zanzibar wanachama wa CHADEMA wampigie mgombea urais wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, kiongozi huyo alidai kusikitishwa na alichozungumza Membe juzi na kwamba kupitia mkutano mkuu wa taifa waliamua kushirikiana na Membe alipokuja katika chama aliambiwa na akakubali kushirikiana katika kampeni.

Juzi, Membe alizungumza na waandishi wa habari na kusema ataendelea na kampeni zake katika ngwe ya mwisho huku akiwakata wapigakura kumchagua wanayeona anafaa.

Maalim Seif alisema baada ya kuona kampeni zinasuasua, walikutana na kushauriana na Membe ambaye aliomba muda wa kutafakari na baadaye walikubaliana kushirikiana na Lissu, lakini ushirikiano wake (Membe) haukuwa mkubwa.

"Nasikitika sana leo (jana) mjumbe (Membe) wa kamati hiyo hiyo anakuja kukana makubaliano yetu," alisema.

"Alilosema Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, si lake na mimi (Maalim Seif) nililosema si langu bali ni uamuzi rasmi wa chama. Mimi ni Mwenyekiti wa Chama, Kamati Kuu na Halmashauri ya Uongozi na moja kati ya majukumu yangu ni kusimamia uamuzi wa chama, ulifanywa tokea kikao cha kwanza kabisa," alifafanua.

**ABAINISHA KASORO**

Aidha, alisema kwa upande wa Zanzibar kuna njama za wazi zilizobainishwa mapema juu ya kuleta kasoro kwenye uchaguzi na yasiposhughulikiwa mapema haitaridhia.

Alisema wananchi wengi watakosa haki yao ya kikatiba ya kupiga kura kutokana na wengi kutoandikishwa na kwamba haki ya kikatiba imeporwa kwa zaidi ya wananchi 1,000.

Aliongeza kuwa wakati wa uteuzi wa wagombea kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) wanachama wa ACT-Wazalendo wanane na 12 wawakilishi walienguliwa.

"Tunavyoambiwa lengo kura ya mapema ni kuwawezesha watu wenye majukumu ya usalama pamoja na ulinzi na usimamizi wa uchaguzi kupata muda wa kusimamia ulinzi na usalama siku ya uchaguzi mkuu, sasa hawa wanaopiga kabla Oktoba 27 hawataruhusiwa kuwapigia Serikali ya Muungano," alisema Mwenyekiti Seif.

Vile vile, alisema katika uchaguzi kumekuwa na vitendo vya kuvunjwa kwa haki za kibinadamu vinavyofanywa na baadhi ya watu kutokana na kukithiri kwa vitisho kiasi cha baadhi ya watu kukimbilia porini.

Kwa mujibu wa Maalim Seif, kuna njama za kumdhibiti baada ya kupiga kura yake ikiwamo kukosa mawasiliano ya simu na viongozi wenzake.

# NEC yaonya kujitangaza mshindi wa uchaguzi

## Orodha ya mawakala yahitajika leo

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema kikundi, taasisi, chama cha siasa au mtu yeyote atakayetangaza matokeo ya uchaguzi mkuu kwa ngazi yoyote kabla ya mamlaka, atachukuliwa hatua stahiki.

Vilevile, imevikumbusha vyama vya siasa kuhakikisha vinawasilisha orodha na barua za utambulisho wa mawakala wa vyama kwa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo husika.

Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu wajibu wa vyama vya siasa na wagombea wakati wa kampeni, uteuzi na mamlaka ya vyama vya siasa na utangazaji wa matokeo.

Alisema NEC inakumbusha kuwa mamlaka za kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais, ubunge na udiwani ni ya tume.

"Kwa msingi huu, atakayefanya hivyo kabla ya mamlaka rasmi zilizowekwa kikatiba na kisheria, atakuwa amevunja sheria na hatua stahiki za kisheria zitapaswa kuchukuliwa dhidi yake," alionya.

Jaji Kaijage alisema tume haitarajii kuona kikundi, taasisi, chama cha siasa, wagombea na wafuasi wao au mtu yeyote akijichukulia sheria mikononi kutangaza matokeo ya uchaguzi nje ya utaratibu na mamlaka zilizowekwa kikatiba.

Katika mkutano wake huo, Jaji Kaijage pia alisema NEC inavipongeza vyama vya siasa na wagombea ambao wanaendelea na kampeni kwa mujibu wa sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi.

**Kwa msingi huu, atakayefanya hivyo kabla ya mamlaka rasmi zilizowekwa kikatiba na kisheria, atakuwa amevunja sheria na hatua stahiki za kisheria zitapaswa kuchukuliwa dhidi yake," alionya.**

HABARI KITAIFA

# JPM ataka Watanzania kukataa ubaguzi

**Na Gwamaka Alipipi, KOROGWE**

ZIKIWA zimebaki siku saba kuelekea uchaguzi mkuu, mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, amewataka Watanzania kujitenga na propaganda za ubaguzi zinazoenezwa na baadhi ya wagombea.

Pia amewatahadharisha Watanzania wakimwona mtu anazungumza na kutangaza chuki, wafahamu kwamba hayupo kwa maslahi ya taifa, bali ana malengo mabaya ya kuleta machafuko nchini.

Alitoa rai hiyo jana wilayani Korogwe mkoani Tanga, wakati akiwahutubia wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza katika Uwanja wa Chuo cha Ualimu Korogwe. Pamoja na mambo mengine, aliwakumbusha Watanzania kuendelea kudumisha amani.

"Wenye roho mbaya watajitokeza kwa sababu wameiona Tanzania imetoka katika umaskini wa mwisho. Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 Afrika ambazo uchumi wake unakua. Tanzania ina mali kila sehemu, watu wanaimezea mate, watafurahi siku moja kuona Watanzania wanapigana ili wao waje kutuuzia silaha huku wakichimba madini," alisema na kuongeza:

"Mkimaliza kupigana mnakuta wamemaliza kila kitu. Lazima Watanzania kujitenga na watu wa propaganda hizo. Wataleta watu wa uchonganishi, wameshashindwa lakini wanahamasisha watu kuandamana."

Magufuli alisema mataifa mengi duniani huwa yanaingia katika machafuko kutokana na kuenezwa kwa uduni, ukabila na umaeneo, hivyo akawataka Watanzania kuwapuuza viongozi wanaohamasisha masuala hayo.

"Wagombea urais tupo 15, ukiona mtu anazungumza na kutangaza chuki ujue hayuko kwa maslahi ya taifa. Mapigano mengi duniani huchonganishwa kwa udini, ukabila au umaeneo, Nawasihi hata vijana wetu ambao hata hamuangalii historia ya taifa hili kuweni watulivu," alisisitiza.

Kuhusu Mkoa wa Tanga, Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali ilitoa Sh. bilioni 55.7 kugharamia elimu bure, Sh. bilioni 17.8 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu, ikiwamo ukarabati wa shule ya wasichana Korogwe.

Dk. Magufuli alisema, katika afya, serikali ilipeleka Sh. bilioni 17.4 kwa ajili ya kujenga jengo la wagonjwa wa dharura na jengo la kuchuja damu kwa wagonjwa wa figo kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo.

Alisema pia serikali imejenga hospitali za wilaya tano ambazo tatu katika Wilaya za Korogwe, Muheza na Tanga Jiji, huku mbili zikiwa katika wilaya za Handeni na Mkinga ambazo ujenzi wake bado unaendelea.

Kuhusu sekta ya maji, Rais Magufuli alisema serikali imetekeleza miradi 64, mjini ikiwa ni miradi 10 na vijijini miradi 54, kwamba miongoni mwa miradi hiyo ni wa Pungwe-Muheza uliogharimu Sh. bilioni 3.07 ambao hadi sasa umefikia asilimia 85.

Alitaja mradi mwingine ni Mkata-Malesi uliogharimu Sh. bilioni 2.53. Alisema mradi wa Mto Pangani kutoka Korogwe-Mheza wenye thamani ya Sh. bilioni 200 utaanza kujengwa mwanzoni mwa mwaka ujao.

Wakati huohuo, Rais Magufuli akiwa wilayani Same mkoani Kilimanjaro alimwagiza mkandarasi anayejenga mradi wa maji wa Bwawa la Nyumba ya Mungu kuongeza kasi ya ujenzi wa bwawa hilo ndani ya siku 30.

Pia alimtaka Mkurugenzi wa Wizara ya Maji, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Waziri, kuhakikisha wanafika katika mradi huo na kumpeleka ripoti.

"Mradi ulitakiwa kukamilika tangu mwaka 2017, haiwezekani hadi leo uwe bado. Haiwezekani wananchi wa Hedaru wazame kisa tatizo la maji, wamesubiri kwa muda mrefu, nawaomba radhi, kwa hiyo kama wapo watu walikula pesa za mradi huo Sh. bilioni 200 waanze kuzitapika kuanzia leo," alisema Dk. Magufuli na kuongeza:

"Nawahakikishia kuwa siwezi kuzungumza uongo, ninafahamu kuzungumza uongo ni dhambi, uwe Waziri au Naibu Waziri au Katibu Mkuu au Mkurugenzi kwa sababu mimi bado ni rais, nataka kesho waende kukagua mradi nikifika Moshi wanileteе ripoti," alisema Dk. Magufuli.

# Mke wa Dk. Salim afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ametuma salamu za pole kwa familia ya Waziri Mkuu mstaafu, Dk. Salim Ahmed Salim, kwa kumpoteza mke wake, Amne Rifai.



Jana, akiwa Mjini Same mkoani Kilimanjaro, Rais Magufuli aliwaomba wananchi waliokuwa katika mkutano wake wa kampeni za uchaguzi mkuu kusimama kwa dakika moja kumwombea kwa Mungu, Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Dk. Salim Ahmed Salim, aliyefariki ghafla asubuhi ya jana.

"Pia tuendelee kumwombea ndugu yetu Salim ambaye bado anaumwa ili Mungu akamponye. Roho ya marehemu mke wa Dk. Salim ipumzike kwa amani na afya ya Dk. Salim ambaye ameugua kwa muda mrefu sasa na hawezi kutembea nayo ikaimarike na ikaponywe na Mwenyezi Mungu. Amin."

Dk. Salim mwenye umri wa 78, alikuwa Waziri Mkuu wa Tanzania kuanzia Aprili 24, mwaka 1984 hadi Novemba 5, mwaka 1985, amewahi kuhudumu kama mwanadiplomasia nguli katika Umoja wa Mataifa (UN).

Pia aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU).

Kiongozi huyo ameshapata nishani mbalimbali za nyota ya Afrika, nishani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nishani ya kitaifa ya Vilima Elfu Moja, nishani ya kipendo (Msalaba Tukufu), ya Sifa (Ofisa Tukufu), Medali ya Afrika, Nishati ya Kitaifa cha Simba (Ofisa Tukufu).

Aidha, alipata nishani ya Miti Miwili ya Naili, nishani ya El-Athir, nishani ya Mono, Masahaba wa O.R. Tambo (Dhahabu), nishani ya Mwenge (daraja la pili).

Aidha, alipata tuzo za heshima kutoka vyuo vikuu mbalimbali za udaktari wa sheria mara mbili, Humanities, Sheria ya Kiraia, Sanaa katika masuala ya Kimataifa na Falsafa katika Uhusiano wa Kimataifa.


NMB
Close to you

## INVITATION TO TENDER

## TENDER FOR PROVISION OF VARIOUS SERVICES FOR NMB BRANCHES ACROSS THE COUNTRY

NMB Bank Plc is the leading commercial bank in Tanzania. The bank has set funds for year 2020, towards the cost of operations and maintenance of its facilities for NMB HQ and its branch network.

It is intended that part of these funds will be applied to eligible payments under contract(s) for provision of various services as per the list below.

- Provision of Fumigation services
- Provision of Cleaning Services
- Provision of Service Maintenance of Fire extinguishers
- Provision of Service and Maintenance of Air Conditions
- Supply of Stationeries and Consumables

NMB Bank Plc intends to engage eligible, qualified and registered local companies/ authorized vendors who will provide the above listed services for its branches and offsite ATMs across the country divided in eight (8) zones as detailed in the tender document.

Interested applicants may download the tender document through NMB Website at this link ***https:// nmbbank.co.tz/tenders.***

The selection of eligible and qualified vendors will be conducted through the open tendering procedures as specified in NMB Bank Plc procurement policy and procedures.

A complete set of tender documents shall be purchased by interested applicants at a non-refundable fee of TSHS 50,000.00 per each category and payment should be done through any NMB branch to NMB Account No. 302040002, account name – Tender Fees (Deposit slip shall be attached when submitting your tender document). Any further clarifications required should be addressed to the secretary NMB Management Tender Committee through this email ***procurement@nmbbank.co.tz***.

All applicants must include one original plus two copies of the tender. The document must be properly filled, and enclosed in plain envelopes hand delivered to NMB Zonal Offices through addresses provided in the tender document not later than **Monday 2nd November 2020 at 15.00HRS**. Applications will be opened promptly thereafter in public and in the presence of applicants' representatives who will choose to attend.

Late tenders, portion of tenders, electronic tenders, tenders not received, and tenders not opened and not read out aloud in public at the bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation.

**The Secretary, Management Tender Committee**
**P.O. Box 9213, Dar es Salaam, Tanzania.**
**NMB Bank Plc. Head Office Ohio/Ali Hassan Mwinyi Street**

215951202

***www.nmbbank.co.tz***

# CCM yataja siri wagombea wake kutoenguliwa NEC

**Na Thobias Mwanakatwe**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimefichua siri kuhusu wagombea wake kutoenguliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu kwa kigezo cha kushindwa kujaza fomu.

Aliyefichua siri hiyo ni Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Bashiru Ally, katika mahojiano na Shirika la Utangazaji la BBC, jana alfajiri kuhusiana na mambo mbalimbali kuelekea uchaguzi mkuu.

Dk. Bashiru alipoulizwa suala la wagombea wengi wa ubunge na udiwani wa upinzani kuenguliwa na NEC na je, CCM ilitumia mbinu gani hadi wagombea wake hata mmoja asienguliwe? Alijibu kuwa siyo suala la mbinu, bali ni suala la kutii na kufuata sheria hasa ikizingatia kuwa uchaguzi nchi zote unasimamiwa na sheria na kanuni.

"Zipo sheria zinazoelekeza namna gani vyama vifanye uteuzi kupitia kwenye mifumo yao ya vyama, viombe uteuzi NEC, namna gani wagombea wake wajaze fomu, muda wa kuchukua na kurejesha fomu," alisema.

Dk. Bashiru alisema kwa upande wa CCM vipo vitengo vya sheria vinavyosimamia na kuruhusu wagombea wa ngazi zote kujaza fomu na kisha kuhakikiwa.

Katika mchakato wa wagombea wa udiwani na ubunge Agosti mwaka huu, NEC iliwaengua wagombea wengi wa upinzani kwa maelezo ya kukiuka masharti ya ujazaji wa fomu.

Hali hiyo ilisababisha CCM ipate wabunge 28 ambao wamepita bila kupingwa, na kwa sasa wanasubiri kuapishwa, baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi.

Hata hivyo, wagombea ubunge na udiwani kupitia upinzani walioenguliwa walikata rufani NEC, ambayo kwa awamu tofauti iliwarejesha baadhi ya walioshinda rufani kuanza kampeni.

Katika hatua nyingine, CCM imelitaka Jeshi la Polisi kuzingatia mafunzo yao na weledi na kutumia nguvu zisizopindukia kiwango katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Dk. Bashiru, alisema hayo alipoulizwa kuwa kumekuwa na hali ya usalama kuteteleka hususani maeneo ambako wapinzani wanafanyia kampeni, polisi wanatumia nguvu kupita kiasi.

Akijibu alisema: "Wito wangu ni jukumu la polisi kuzingatia mafunzo yao na weledi na kutumia nguvu zisizopindukia kiwango."

Hata hivyo, Dk. Bashiru alisema katika kipindi hiki wananchi wahakikishe wanatii sheria bila shuruti kwa sababu polisi wana mafunzo ambayo yanawafanya watathmini hali ilivyo na kuchukua hatua.

"Wapo wagombea wanajua sheria, mwisho wa kufanya kampeni ni saa 12:00 jioni, hiyo siyo sheria ngeni, lakini unakuta mgombea anafanya mkutano na wafuasi wake saa 2:00 usiku," alisema.

Alisema tabia za namna hiyo za kuvunja kanuni za maadili ya uchaguzi zitaweza kuwa chanzo cha matatizo kama hayo.

Dk. Bashiru akijibu swali aliloulizwa kwamba wapo baadhi ya watu wanajisikia kutokuwa huru nchini,

alisema hakuna mahali popote uhuru ukawa ni shibe iliyokamilika, kila nchi duniani kuna madai ya upeo wa uhuru, hivyo hakuna jamii itatosheka na uhuru huo.




Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, Francis Luena (kulia), akikabidhi Sh. milioni 8.1 kwa mwalimu mstaafu Elias Mihambo Katinda, mjini Shinyanga jana, kati ya Sh. milioni 45 alizodhulumiwa na mikopo umiza. Sh. milioni 18.5 alishakabidhiwa awali, na kusalia Sh. milioni 18.2 zinazoendelea kufuatiliwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TAKUKURU yarejeshea wastaafu mamilioni waliyoporwa kwa mkopo

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, imewarejeshea walimu wastaafu wawili Sh. milioni 16.6 ambao waliathirika na mikopo umiza.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Hussein Mussa, alibainisha hayo jana wakati akisoma taarifa ya taasisi hiyo kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2020/21), kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Alisema wameendelea kufanya kazi ya kusaidia wananchi ambao wamekuwa wakitapeliwa na mikopo umiza pamoja na wale ambao wanaombwa rushwa kwa ajili ya kupewa huduma za kijamii.

Katika kufanya hivyo, Mussa alisema wameokoa Sh. milioni 27 ziliwamo Sh. milioni 16.6 za walimu.

"Mstaafu wa kwanza, Elias Mihambo, tumemrejeshea leo (jana) Sh. milioni 8.1 kati ya Sh. milioni 45 ambazo alitapeliwa na mikopo umiza. Awali tulimpatia Sh. milioni 18.5 na kusalia milioni 18.2," alisema Mussa.

"Mstaafu wa pili, Hamis Maziku, tumemrejeshea naye Sh. milioni 8.5 kati ya Sh. milioni 27.5 ambazo alitapeliwa na mikopo umiza. Awali tulishampatia Sh. milioni nane na kusalia Sh. milioni 11. Fedha zote hizi bado tunazifuatilia ili walipwe zote," aliongeza.

Pia alisema wamemrejeshea Sh. milioni 10.4 Jacksoni Njau ambazo alidhulumiwa na kamishna msaidizi wa ardhi mkoani Mwanza, aliyemwomba kwa ajili ya kumpimia ardhi (shamba) ekari 23 lililoko Pandagichiza wilayani Shinyanga pamoja na kumpatia hati miliki, lakini hakufanya hivyo na kukata mawasiliano naye.

Wanufaika waliorejeshewa fedha zao, wakizungumza kwa nyakati tofauti, walishukuru TAKUKURU kwa kazi nzuri ambayo imeifanya kwa kuokoa fedha zao ambazo zilichukuliwa isivyo halali kutokana na wao kuandamwa na shida kipindi hicho.

# Wakazi Tandale walalama ukatili

**Na Elizabeth Zaya**

WAKAZI wa Tandale kwa Tumbo, Kinondoni jijini Dar es Salaam, wamewaomba wanaume kuungana na makundi mengine katika jamii kupambana na vitendo vya ukatili katika jamii yao.

Wakazi hao walitoa ombi hilo walipotembelewa na Shirika la Mabadiliko la Kujenga Ushirikiano kwa Wote (TIBA), katika vijiwe vya kahawa ambavyo wanaume hupendelea kukusanyika nyakati za mapumziko baada ya shughuli zao.

Winie Mwangosi, mmoja wa wakazi wa eneo hilo, alisema asilimia kubwa ya vitendo vya ukatili vinavyotokea katika eneo hilo, wanawake ndio huwa mstari wa mbele kuvikemea, huku wanaume wakijiweka pembeni.

Mwenyekiti wa mtaa huo wa Tandale kwa Tumbo, Khatibu Kibwana, alisema amekuwa akipokea taarifa nyingi za ukatili huo na vingi vikitokana na vipigo.

"Ni kweli katika mtaa wetu tumekuwa tukipata taarifa nyingi za ukatili, ambao unagusa pande zote za wanawake na wanaume na vinatokana na vipigo, na wengi wanafanya vitendo hivyo nyakati za usiku wanapokuwa wamelewa," alisema Kibwana.

"Na kukomesha vitendo hivi katika eneo letu inakuwa ngumu kwa sababu huwa tunakosa ushirikiano wa upande mmoja wa wanaume, wanawake ni wepesi sana kutoa ushirikiano."

Ofisa Ustawi wa Jamii wa mtaa huo, Hyness Charles, alisema kwa siku hupokea taarifa za vitendo vya ukatili kuanzia saba hadi 10.

"Na ukihoji vitendo vingi vya ukatili vinavyojitokeza katika eneo hili ni vile vinavyotokana na vipigo na tumekuwa tukipambana sana kuvikemea kwa kuwafikisha katika vyombo vya sheria watuhumiwa wanaoripotiwa, lakini tatizo tunakosa ushirikiano wa ushahidi kutoka kwa wananchi hususani wanaume," alisema Hyness.

Mkurugenzi wa Shirika la TIBA, Malcela Lungu, alisema kuna haja ya kila mmoja katika jamii kushirikiana kwa pamoja kutokomeza vitendo hivyo.

Malcela alisema suala la mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili ni la lazima liwe la kushirikiana.

"Jamani tuondokane na fikra potofu kwamba kukemea vitendo hivi ni kazi ya wanawake tu, hili siyo sawa kwa sababu tunashuhudia makundi yote yanaathirika na tukumbuke kuwa katika familia au jamii anapoathirika mtu mmoja amepunguza nguvu kazi na kurudisha maendeleo nyuma, na tukilitambua hili sisi sote tutawajibika kuvikemea," alisema Malcela.

"Na tunaendelea kuwasisitiza wanaume kuamka na wao, wasiwaachie wanawake tu kwa sababu nao wanaathirika."

Malcela alisema TIBA, wataendelea kutoa elimu katika makundi mbalimbali ya jamii ili kuhakikisha kila mmoja anafahamu wajibu wake katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo vya ukatili.

## HABARI KITAIFA

# Matukio moto shuleni yamwibua CAG Assad

**Na Woinde Shizza, MWANGA**

MFULULIZO wa matukio ya kungungua moto shule za Kiislamu katika mikoa mbalimbali nchini, umemwibua aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Musa Assad, kuzungumzia vitendo hivyo, akiomba kuundwa kwa kamati maalum ya uchunguzi itakayofuatilia mikasa hiyo.

Akizungumza jana katika mahafali ya sita ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Kiislamu ya Vuchama, Ugweno, Wilaya ya Mwanga, alisema huenda matukio hayo yanasababishwa na wivu wa maendeleo.

"Mimi nadhani kuna haja ya kuiomba serikali ije na kamati ya uchunguzi wa moto katika shule za kiislamu, ifanye uchunguzi wa kina na kubaini chanzo cha matukio yanayoendelea hivi sasa.

"Kuna shida nyingine, kwamba tatizo Kikosi cha Zimamoto na Ukoaji hakina wataalamu wa kutosha wa kukabiliana na majanga ya moto na hii lazima iangaliwe upya na kama hatuna wajuzi, tuagize kutoka nje ya nchi ili ijulikane na watu wakatoa hofu."

Kwa mwaka huu, Mkoa wa Kilimanjaro peke yake kumejitokeza matukio ya moto katika seminari ya Kiislamu ya Mudio (Hai), mabweni ya Shule ya Seminari ya Wasichana ya Kiislamu ya Kaloleni (Moshi Mjini), Shule ya Sekondari Uchira Islamic (Moshi Vijijini) na Chuo cha Quran cha Hadithi za Mtume cha Othuman Bin Halfan (Hai).

Prof. Assad alieleza kuwa mfululizo wa matukio hayo ya moto kwa shule za Kiislamu nchini unaacha maswali yasiyojibika, hasa baada ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini kushindwa kubaini chanzo cha moto huo.

Kutokana na majanga hayo, Prof. Assad, ameshauri wamiliki wa shule zote za Kiislamu kuimarisha ulinzi wake kwa kufunga kamera za usalama (CCTV), ili kusaidia kubaini chanzo cha matukio hayo.

Awali, akitoa taarifa ya Sekondari Vuchama, meneja wa shule hiyo, Yasin Mfinaga, alisema tayari serikali mkoani Kilimanjaro, imetoa maelekezo ya namna ya kujikinga na majanga hayo.

"Sasa sisi kama uongozi wa shule, tumechukua tahadhari ya kijipanga kwa kutoa ulinzi katika shule yetu, lakini niombe serikali ijikite kufanya uchunguzi wa kina ili kuwatoa hofu wazazi na wanafunzi," alieleza Mfinanga.

Wakati, Mkuu wa shule hiyo, Jumanne Mkoga, akizungumzia maendeleo ya shule, alisema kuwa Shule ya Sekondari ya Vuchama, imekuwa ikifanya vizuri kitaaluma tangu ilipoanzishwa mwaka 2015, ikishika nafasi za juu kiwilaya na mkoa na haijawahi kuwa na wanafunzi wanaopata alama sifuri kwenye ufaulu.

## Mgombea urais UPDP ataka wenzake wayakubali matokeo

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kupitia UPDP, Twalib Kadege, amewataka wagombea urais wa vyama vyote vya siasa kukubali mshindi wa nafasi hiyo atakayetangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Amesema NEC ndiyo yenye mamlaka ya kisheria ya kufanya hivyo, ili kudumisha amani na utulivu katika nchi.

Alisema hayo jana wakati akizungumza katika mahojiano na gazeti hili kuhusu mtazamo wake wa mwenendo wa kampeni baada ya kubakia siku saba kabla ya kupiga kura Oktoba 28, mwaka huu.

"Ni vizuri vyama tuwe na desturi tukubali kushindwa, kwa sababu katika wagombea 15 wa urais haiwezekani wote wakashinda, yule ambaye atatangazwa na NEC tumkubali maana ndio kazi yake kumtangaza aliyeshinda si kazi ya NEC kumtangaza mtu aliyeshindwa," alidai.

Kadege ambaye amekuwa kimya bila kufanya kampeni, alidai ana imani kubwa na NEC kwani haijaonyesha dalili za upendeleo wa chama wala mgombea yeyote, hivyo itatenda haki kwa kumtangaza mgombea atakayeshinda kwa kupigiwa kura na wananchi.

"Kama ukiona kwamba haujachagulika ujue kura hazikutosha, kwa hiyo usilazimishe kwamba umeibiwa kura bila kuwa na uthibitisho, maana kufanya hivyo ndio chanzo cha kuzuka kwa vurugu," alidai.

Kadege alisema wagombea lazima watambue kuwa wananchi kujaa kwenye mikutano yao ya kampeni haina maana kwamba watawapigia kura wote wapo wengine wanakwenda kusikiliza tu sera, lakini sio wapigakura.

"Ambaye sera zake hazitakubalika basi akubali wananchi hawakuridhia na sera zake, hivyo angoje awamu inayofuata, hakuna haja ya kuleta vurugu wala fujo na maneno yasiyokuwa na tija," alisema.


IITA
Transforming African Agriculture
50 1967-2017

**POSITION ANNOUNCEMENT**
**FIELD ASSISTANT**
**IITA-TZ-2020-NRS-004-NRS-DSM**

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the following position of Field Assistant to support the IITA banana project based at the IITA Office at the Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NMAIST) in Kijenge, Arusha

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future

**Responsibilities:**

- Coordinate and manage experimental design, plot layout, planting, weed control and trial management, including supervision of field operation.
- Supervise and/or conduct field data collection, computer data entry and analysis, synthesis and writing report.
- Coordinate integrated work of field breeding program and supporting laboratory technician to maximize breeding efficiency
- Coordinate field labour and research assistant working on trials for which he/she has responsibility.
- Assist the supervisor in the procurement of goods (scientific and nonscientific)

**Required Qualifications / Experience**

- BSc in Horticulture, Agronomy and work in Agriculture related fields with at least 2 years' experience
- Ability to work independently with minimal supervision, but also participate as a team member in accomplishment of duties.
- Strong attention to detail
- Possess excellent interpersonal and communication skills in English
- Ability to work in a multi-cultural environment.
- The ability to work independently and as a team member;
- A positive attitude.

The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Dar es salaam. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

Applications: Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to IITA-Tanzania@cgiar.org

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.

**Closing date: Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.**
**Please note that only shortlisted candidates will be contacted.**

215950802

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Kila mwananchi atambue kura yake ina thamani kubwa*

ZIMEBAKI siku saba ili kila Mtanzania afanye maamuzi ya mwisho ya nani anafaa kuwa diwani, mbunge na rais kwa miaka mitano ijayo.

Kura ni siri na hakuna yeyote atakayejua umempigia kura nani, hivyo anayekwenda kupiga kura ampigie ambaye amemridhisha kwa sera na mipango yake, asiangalie amempa rushwa ya chakula, mali au fedha.

Kama mtu atachagua kiongozi kwa kuwa amempa kitu, maana yake ameuza kura yake na itamgharimu maisha yake kwa miaka mitano ijayo.

Kila chama kwa sasa kipo katika ng'we ya mwisho ya kushawishi wapigakura kwa kutoa ahadi kuonyesha kwamba ndiye mgombea sahihi dhidi ya mwingine.

Katika nafasi ya urais kuna wagombea 15 kutoka vyama, na kila mmoja anafanya kampeni sehemu mbalimbali kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Kwa sasa kila mgombea hususan wa urais anapambana, huku wengine wakitumia chopa kuwafikia wapiga kura kwa haraka na kufanya mikutano mingi kwa wakati mmoja.

Ahadi na sera nyingi zimemwangwa kwa wananchi na baadhi ya vyama kama CHADEMA, CCM, ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi na CUF, vimeweka wazi ilani zao na wananchi wamezisoma na wengine wameenda mbali zaidi na kuziweka mtandaoni.

Ilani za vyama ndiyo mwongozo wa yote ambayo vyama hivyo vikiingia madarakani vitatekeleza katika sekta mbalimbali, na vyama hivyo vimeeleza vipaumbele vyao, ikiwamo mambo ya kwanza watakayofanya baada ya kuingia madarakani.

Kwa CCM ilani yake imeonyesha yaliyofanyika kwa kipindi cha miaka mitano, na yatakayofanyika miaka mitano ijayo.

Aidha, vyama vya upinzani ndiyo vinaomba ridhaa ya kuingia Ikulu kwa mara ya kwanza, vina ahadi nyingi na matumaini megi kwa wananchi kama njia ya kuwashawishi ili wapate nafasi husika.

Kupiga kura ni haki ya kikatiba kwa kila Mtanzania aliyepo kwenye daftari la kudumu la wapigakura lililotolewa na NEC na ZEC, na siku hiyo kila mtu atapiga kura katika kituo alichojiandikishia na kama alihakiki taarifa zake kujua kuwa zipo kwenye kituo husika.

Aidha, katika tovuti ya NEC na ZEC kuna utaratibu wa mpigakura kuhakiki taarifa zake kupitia simu yake, ambayo humwonyesha kama jina lake lipo katika daftari na katika kituo gani ambacho atapiga kura.

Ni wajibu wa kila mmoja kufanya maamuzi sahihi kwa wakati sahihi kwa ajili ya maisha yake ya miaka mitano ijayo.

Tunawasihi wananchi kujitokeza kwa wingi kutimiza wajibu wa kikatiba, mwananchi usikubali kuharibu kura yako au kuacha kupiga kura kwamba watu wengine wakuamulie kiongozi gani anafaa.

Ni lazima kila mmoja ashiriki na ahakikishe kura yake ni sahihi asiharibu kura, na tunaposema kuharibu kura ni kuweka tiki nje ya sanduku la mgombea la kuweka alama ya vyema au kutiki zaidi ya mgombea mmoja.

Wapigakura wanapopewa karatasi ya kupiga kura ni lazima awe ameshafanya maamuzi atamchagua nani kwa kuweka tiki au alama ya vyema kwenye eneo la mgombea husika, ili awe ameshiriki katika maamuzi sahihi ya kiongozi amtakaye.

Kama ambavyo wamekuja kuomba kuchaguliwa kutuwakilisha katika Baraza la Madiwani la Halmashauri na Manispaa kwa ajili ya kuzisema kero na changamoto mbalimbali za maeneo mengine.


Na siku hiyo ndiyo wananchi watachagua mwakilishi wa jimbo ambaye ataingia katika mhimili wa Bunge au Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutunga sheria na kuisimamia serikali ili iweze kuwajibika kwa wananchi.

Kulalamika, kulia juu ya mambo mbalimbali ambayo ungetamani yabadilike hakutasaidia kitu, iwapo hutashiriki kupiga kura kwa kiongozi umtakaye.

Oktoba 28, mwaka huu, ni siku muhimu kwa kila mmoja kufanya maamuzi sahihi kwa kiongozi sahihi wa kumwakilisha katika ngazi mbalimbali za maamuzi, kura moja inathamani kubwa ina inaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Inapobakia wiki moja ni vyema kuzingatia haya

WAKATI limebakia juma moja kuelekea kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika wiki ijayo Jumatano Oktoba 28, yapo masuala ya kukumbushana.

Ni yale ambayo kimsingi mpigakura anahitaji kuyafahamu kulingana na sheria, kanuni na miongozo ya uchaguzi pamoja na maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

NEC katika taarifa yake kuhusu majukumu ya tume na taratibu za uchaguzi, zilizotolewa Agosti mwaka huu, inaeleza kwamba mpigakura aliye na sifa ya kufika kwenye kituo ili kupiga kura yake ni yule aliyejiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura.

Pia mwenye haki anatakiwa pia kuwa na kadi ya kupigia kura au awe na kitambulisho cha uraia (cha taifa), leseni au pasipoti, kulingana na tangazo la NEC lililotolewa wiki hii.

Vilevile mpigakura sharti awe mkazi wa eneo analopigia kura, ikiwa alihama eneo lake awe ametoa taarifa zake ili apige katika kituo kingine cha makazi mapya.

Taratibu za kupiga kura zinaeleza kuwa kabla ya muda wa kuanza upigaji kura, msimamizi au msaidizi wake katika kituo cha kupigia kura atafungua sanduku la kuhifadhia kura na kuonyesha mawakala wote na wahusika wengine, ili kuthibitisha hayana kitu ndani.

Pia mpigakura kabla ya kupiga kura atatakiwa kukabidhi kadi yake kwa msimamizi huyo ili kuhakiki jina na kukabidhiwa karatasi ya kupigia kura akimaliza atakusanya karatasi katika masanduku.

Pia mpigakura anapaswa kufahamu kwamba, ni kosa la jinai kujaribu kupiga kura zaidi ya mara moja katika uchaguzi na kutumia kadi ya mtu mwingine.

Pia mpigakura hatakiwi kuchana orodha ya wapigakura au mabango ya elimu kuhusu mpigakura yaliyowekwa vituoni.

Pia NEC inasisitiza kuwa kuvaa nguo za wagombea, kubeba picha zao au kufanya kampeni kunadi chama fulani cha siasa, ni kinyume cha utaratibu siku ya kupigakura.

Kulingana na taratibu za NEC, muda wa kuanza kupiga kura ni kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 10 jioni kwa upande wa Tanzania Bara, wakati Zanzibar vituo vitafunguliwa saa moja asubuhi na kufungwa sa 11 jioni.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaeleza kuwa Tanzania inatumia mfumo wa uchaguzi ambao mgombea anayepata kura nyingi halali kuliko wengine ndiye hutangazwa mshindi.

Ni kwa mujibu wa kifungu cha 35 F(8) cha ibara ya 41(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 81(a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, sura ya 292.

Inaeleza kuwa uchaguzi wa wabunge, wanawake watakaofuatwa na vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi, vitapendekeza kwa NEC majina ya wanawake kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa uwakilishi baina ya vyama vilivyoshinda katika majimbo na kupata viti bungeni. NEC ikiridhika kuwa yeyote aliyependekezwa anazo sifa za kuwa mbunge itamtangaza kuwa amechaguliwa kuwa mbunge.

Aidha, NEC inaelekeza kuwa ni marufuku kwa mgombea au chama kujitangazia ushindi kabla ya chombo hicho, kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na hatua zinachukuliwa dhidi ya mhusika.

Lakini wapigakura wanashauriwa kupigakura na kurudi nyumbani au kuendelea na shughuli zao badala ya kukaa karibu na kituo kwa madai kuwa wanalinda kura.

Wakati mwingine licha ya kwamba wananchi wangependa kuona mgombea wao anashinda ni vyema kutii sheria na maelekezo ya uchaguzi jukumu hilo lifanyike kwa amani, utulivu na kwa haki.

Aidha, ikumbukwe kuwa kuna maisha baada ya kupigakura kwani wananchi hurejea tena kwenye majukumu yao, wakati tume hufanya shughuli ya tathmini ikiwamo kushughulikia kesi za uchaguzi, kuandaa taarifa na marekebisho ya sheria pale yanapohitajika.

## HABARI KITAIFA

# Jela miaka 30 kumbaka mtoto kwa zamu

**Na Samson Chacha, TARIME**

WAKAZI wawili wilayani hapa, Samwel Tengaga (20) na Jaffari Msuka (20), wamehukumiwa kwenda jela kila mmoja miaka 30 baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka binti wa miaka 16 kwa zamu.

Walisomewa hukumu hiyo juzi mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya Tarime, Visencia Balyaruha, baada ya mahakama hiyo kuwapata na hatia kutokana na ushahidi wa upande wa mashtaka uliotolewa mbele ya mahakama hiyo.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Dhabiti Matembo, alidai kuwa watuhumiwa kwa pamoja wakiwa katika Kijiji cha Buriba, Kata ya Sirari, Mei 6, mwaka huu usiku saa mbili, walimkamata kwa nguvu binti wa miaka 16 na na kumbaka kwa zamu na kumsababishia maumivu makali.

**Awali, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Dhabiti Matembo, alidai kuwa watuhumiwa kwa pamoja wakiwa katika Kijiji cha Buriba, Kata ya Sirari...**

Katika kesi hiyo upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi watatu na washtakiwa walijitetea wenyewe.

Baada ya hukumu hiyo washtakiwa waliiomba mahakama kuwaonea huruma kwa kuwapunguzia adhabu.

Mwendesha Mashtaka wa Polisi, aliiomba mahakama itoe adhabu kali kwa washtakiwa ili iwe fundisho kwa wengine wenye nia mbaya kama hiyo.

Hakimu Visencia aliwahukumu kila mmoja kwenda Jela miaka 30.

# Familia 600 kukabidhiwa nyumba

**Na Emmanuel Mwamakinga, TUDARCo**

KAYA 656 zinatarajiwa kukabidhiwa nyumba zilizojengwa na serikali katika mradi wa Magomeni jijini Dar es Salaam Januari mwakani.

Mradi huo unaotekelezwa baada ya serikali kubomoa nyumba zilizokuwa kwenye eneo hilo ili kujenga nyumba za kisasa, umefikia asilimia 81.

Baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi huo jana, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga, alisema wanatarajia kukabidhi nyumba hizo kwa wananchi mwanzoni mwa mwaka ujao.

Alisema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 81 na tayari mtendaji mkuu wa mradi huo ameshamthibitishia kukamilika kwa mradi huo ifikapo Januari mwakani.

"Mradi huu unaenda vizuri sana na ninaamini hadi kufikia Januari utakuwa umekamilika kama alivyosema Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). "Wananchi wenye haki zao watakabidhiwa nyumba kwa ajili ya kaya zao bila tatizo kama ilivyoahidiwa serikali ilipoamua kufanya maboresho katika nyumba hizi. "Tunajitahidi kuweka huduma za msingi pamoja na kuiweka nyumba katika mazingira salama zaidi na niwaambie tu ukweli, nimeamua kufanya ziara hii baada ya kupokea simu nyingi kutoka kwa wananchi ambao wanasubiri nyumba zao kukamilika na wengi wanaishukuru serikali na wanaunga mkono juhudi za serikali hii," alisema.

Mtendaji huo wa wizara, alisema mradi huo ulisimama kwa muda kutokana na masuala ya kifedha, lakini mwezi uliopita, serikali ilitoa Sh. bilioni tisa ili kuukamilisha. "Mradi wetu huu ulisimama kwa muda kipindi cha hapa katikati, lakini serikali imetoa pesa nyingi kiasi cha bilioni tisa ili kukamilisha mradi huu. Kwa Sasa hakuna kisingizio tena, wachape kazi usiku na mchana, Januari watukabidhi kama walivyosema," aliagiza.

Daudi Kondoro, Mtendaji Mkuu wa TBA, alisema watafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha hadi kufikia Januari mradi huo uwe umekamilika na wanakabidhi kazi hiyo kwa serikali.

# Tanzania yapaa hali ya hewa kimataifa

**Na Faustine Feliciane**

TANZANIA ni moja ya nchi inayopiga hatua kubwa kwenye masuala ya utabiri wa hali ya hewa na kuchukuliwa kama nchi ya mfano na Shirika la Hali ya Hewa la Dunia (WMO).

Hayo yalielezwa jana na Rais wa tatu wa shirika hilo, Dk. Agnes Kijazi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana wakati wa ufungaji wa warasha ya wanahabari kuelekea utabiri wa mvua kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka, Dk. Kijazi ambaye ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), alisema tangu alipochaguliwa kwenye nafasi hiyo mwaka jana, Tanzania inapewaheshima kwenye shirika hilo duniani na pia imekuwa ikisifiwa kwa shughuli zake.

"Mimi nipo pale kwa ajili ya kuwakilisha dunia nzima na si Afrika au Tanzania peke yake, lakini nisema tu uwakilishi wangu una matokeo chanya, kwa sasa Tanzania inatajwa miongoni mwa nchi zimekuwa zikitolewa mfano kutoka Afrika kwenye masuala haya ya hali ya hewa," alisema Dk. Kijazi.

Aidha, alisema WMO imekuwa ikifuatilia kwa karibu taarifa za TMA na wanasifu utabiri wa hali ya hewa unavyoenda hasa kwa kuongezeka kwa usahihi wa utabiri unaotolewa.

"Lakini niseme tu heshima tunayoipata sasa kimataifa pia inatokana na ushirikiano mzuri tunaoupata kutoka serikalini," alisema.

Katika hatua nyingine, TMA leo inatarajia kutoa utabiri mwingine wa mvua kwa mikoa ya Tanzania Bara inayopata mvua mara moja kwa mwaka.

Mikoa hiyo inayopata mvua mara moja kwa mwaka ni Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Mbeya, Singida, Songwe, Njombe, Iringa, Lindi na Mtwara.


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe | Nipashe mwendo mdundo
Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)
PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store | Google Play
KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz | nipashe | TheGuardiantz | YouTube TheGuardiantz




Mgombea ubunge Jimbo la Arusha Mjini, kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Shangay, akifanya kampeni za uchaguzi katika vijiwe vya kahawa kwenye soko kuu la jijini humo jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wakulima walia bei kiduchu pamba

**Na Happy Severine, BARIADI**

BODI ya Pamba Tanzania (TCB) imesema wakulima na wadau wengi wa pamba wameendelea kulalamikia bei ya zao hilo kuwa ndogo kila mwaka.

Aidha, imeelezwa kuwa ikiwa tija itaongezwa katika uzalishaji wa zao hilo, hakuna mkulima wala mdau yeyote ambaye atalalamikia bei wala hakutakuwa na haja ya kuongeza eneo la uzalishaji wa pamba nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Marco Mtunga, alisema hayo jana kwenye mkutano wa wadau wa pamba uliofanyika mjini hapa kwa lengo la kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango mkakati wa mageuzi ya pamba mkoani hapa.

Mtunga alisema suala la tija katika pamba nchini bado ni tatizo kubwa kutokana na wakulima kutofuata kanuni bora za kilimo, kutopatikana pembejeo kwa muda mwafaka na uwapo wa huduma hafifu za ugani.

Alisema endapo wakulima watafuata kanuni bora za kilimo, pembejeo kupatikana kwa wakati, huduma za ugani kuboreshwa na kutumika ipasavyo mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), tija katika kilimo cha pamba itaongezeka.

Kwa mujibu wa Mtunga, mpaka sasa asilimia 70 ya wakulima wa pamba wanapanda mbegu kwa mstari huku asilimia 30 wakiendelea kupanda kienyeji na kwamba tatizo kubwa ni upatikanaji wa pembejeo kutokana na kufutwa kwa Mfuko wa Kuendeleza Pamba (CDTF).

"Tulifanya maamuzi (uamuzi) ya (wa) kufuta mfuko huu, ambapo madhara yake ndiyo haya leo tunapata. Kila siku wakulima walalamikia hawana mbegu, hawama dawa (dawa) na zikipatikana zinakuja zimechelewa. Yote haya ni kwa sababu ya kufutwa kwa CDTF," alisema Mtunga.

Aliongeza kuwa fedha ambazo zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya pembejeo ni kidogo ikilinganishwa na zile ambazo zilikuwa zikitengwa kwa ajili ya mfuko huo ambao ulikuwa maalumu kusambaza mahitaji hayo kwa wakulima kwa wakati na kutosheleza.

Kuhusu huduma za ugani, Mtunga alisema wakulima wengi wamekuwa hawafikiwi ipasavyo na maofisa ugani kutokana na kutokuwapo kwa vitenda kazi kwa maofisa hao vya kuwafikia kwa haraka wakulima.

Alisema halmashauri licha ya kupata ushuru kupitia zao hilo, bado zimeshindwa kutenga bajeti ya kuwasaidia maofisa ugani kuwanunulia usafiri na kuwatengea bajeti ya kuhakikisha wanawafikia wakulima wengi zaidi.

"Kuna halmashauri zinapata ushuru hadi Sh. bilioni 1, lakini hakuna sheria ambayo inambana mkurugenzi kuhakikisha kwenye huo ushuru anatenga kiasi bajeti kwa ajili ya shughuli za ugani," alisema Mtunga.

Aidha, alisema ili kuongeza tija, lazima mkulima akopeshwe pembejeo na kwamba katika kufanikisha hilo, lazima mfumo wa TEHAMA utekelezwe ipasavyo ili mkulima akikopeshwa akatwe moja kwa moja na mfumo pindi atakapouza pamba na siyo kuanza kumsaka kama ilivyo sasa.

Katika kikao hicho baadhi ya wadau waliitaka serikali kusimamia kwa vitendo baadhi ya maamuzi ambayo yamekuwa yakitolewa na wadau wa zao hilo kwenye vikao mbalimbali ili kuweza kuendeleza zao hilo.


**ELITE BROTHERS LIMITED**
S. L. P 148, DAR ES SALAAM
NAMBA YA KAMPUNI: 141702807

**TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI KWA HIYARI**

Wamiliki wa Kampuni ya **Elite Brothers Limited** yenye Namba ya Usajili **141702807 ya tarehe 18/05/2020** wanapenda kuutangazia uma kuwa, kutokana na kushindwa kuanza biashara miezi mitano baada ya kusajiliwa BRELA na kukosa namna yoyote ile ya kuweza kujiendesha, tumeamua kuifunga kampuni kwa hiyari toka tarehe **17 October 2020**

MOSES COSMAS NYENZA
Mwenyekiti

JAMES SAMWEL MOSHI
Katibu

115951602


# Mgogoro wa ardhi miaka 20 kanisa, bibi wafikia tamati

**Na Munir Shemweta, TABORA**

OFISI ya Ardhi Mkoa wa Tanga imemaliza mgogoro wa ardhi uliodumu kwa zaidi ya miaka 20 kati ya Kanisa la Evangelistic Assemblies of God (EAGT) na Tamasha Mhanuka kwenye eneo la mtaa wa Bakari, Manispaa ya Tabora na kumkabidhi hati.

Mhanuka kwa muda mrefu amekuwa na mgogoro na kanisa hilo lililotaka kulichukua eneo hilo na maeneo ya wakazi wengine watano kwa ajili ya kuendesha shughuli za kanisa. Hata hivyo, wamiliki wa maeneo hayo walishindwa kukubaliana na kanisa kuhusiana na fidia ya kuwaondoa.

Timu ya Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Tabora ikiongozwa na Kamishna Msaidizi wa Ardhi, Jabir Singano, juzi ilikwenda eneo la Mhanuka liliko barabara ya Kigoma na kumkabidhi hati ya ardhi sambamba na kumwonyesha mipaka ya eneo lake ili kufanya maendelezo aliyoshindwa kufanya kutokana na mgogoro huo.

Mkuu wa Idara ya Ardhi Manispaa ya Tabora, Deo Msilu, alisema mgogoro huo ulisababishwa na eneo hilo kuwa katika mpango wa matumizi ya umma, yaani taasisi za dini na kupewa kanisa la EAGT.

Kwa mujibu wa Msilu, kilichotakiwa kufanyika ni uthamini wa kumlipa Mhanuka, pamoja na wakazi wengine watano, aliyekataa kuchukua fidia jambo lililosababisha ofisi ya ardhi mkoa kubadilisha mpango wa matumizi ya eneo hilo na kuwa makazi.

Singano alisema ofisi yake imekuwa ikishirika kutatua migogoro ya ardhi katika mkoa huo na moja ya mgogoro uliofanyiwa kazi ni wa Mhanuka na EAGT.

Singano alisema mgogoro huo awali ulishughulikiwa na Manispaa ya Tabora, lakini haukupata ufumbuzi, jambo lililoifanya ofisi yake baada ya kuanza kazi kuushughulikia.

"Eneo la huyu bibi zuri kama mnavyoona liko katika barabara kuu ya kwenda Kigoma na ni barabara ya lami na stendi iko umbali wa takriban kilometa moja. Tuliliita kanisa na kuzungumza nalo ingawa kuna baadhi ya vipande lililipa fidia lakini kwa kuwa eneo hili lilikuwa utoaji binafsi ilibidi waachwe," alisema.

Baada ya kufikia mwafaka na pande zote mbili, alisema waliamua kupima viwanja vitano na kuwaandalia ankara ya malipo wamiliki wake ili watakapokamilisha wapatiwe hati na kumshukuru Mungu kwa kufanikisha kutatua mgogoro huo alioueleza kuwa ulikuwa ukimfanya Mhanuka kushindwa kufanya maendelezo ya eneo kutokana na kutojua mipaka.

Naye Mhanuka aliishukuru ofisi ya adhi Mkoa wa Tabora hasa Kamishna Msaidizi Singano na Ofisa Mipango Miji, Faraji Shemgha, kwa kusaidia kutatua mgogoro huo na kufanikisha kupatiwa hati.

Hata hivyo, aliiomba serikali na wananchi wenye uwezo kumsaidia kufanikisha ujenzi wa nyumba yake aliyoieleza kuwa haiko katika hali nzuri.


KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

DAR ES SALAAM

UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI

MIRATHI Na. ....77...... YA MWAKA 2020...

MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU

Joyce Stanley Sichone

MWOMBAJI/WAOMBAJI

Jeremiah Godfrey Mwanjoka

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 9th Mwezi wa Novemba ~~2016~~ 2020

Imewasilishwa Dar es Salaam, leo tarehe 9th Mwezi wa Oktoba ~~2016~~ 2020

NAIBU MSAJILI
Deputy Registrar
High Court of Tanzania
Dar es Salaam Zone

NAKALA KWA:
Nipashe Newspaper
.................................
.................................

215951802

# VETA yawezesha mafundi 16,000 kuwa wasomi

**Na Beatrice Moses,** TUDARCo

MAFUNDI wasio na mafunzo rasmi nchini 16,000 wamefanikiwa kufuzu mitihani ya kurasimishwa kupitia utaratibu maalum wa urasimishaji ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi (RPL) unaotolewa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Dk. Pancras Bujulu, aliyasema hayo juzi wakati akiwa kwenye mkutano maalum na waandishi wa habari kutoka Chama cha Waandishi wa Habari jijini Dar es Salam (DCPC) alisema hatua hiyo imelenga katika kuwajengea uwezo wa kushindana kwenye soko la ajira.

Alisema hadi sasa urasimishaji huo unafanywa na VETA kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu umepokelewa vyema, kwani mafundi hao waliojifunza kwa urafiki ama undugu wamejitambua na kuona umuhimu wa kujirasimisha kwa kupewa mafunzo hatimaye kutunukiwa vyeti.

Alisema mpango huo upo nchi nzima, ambapo mafundi waliopata ujuzi kupitia mfumo usio rasmi hufanyiwa tathmini kulingana na ufundi walionao, baada ya hatua hiyo hupewa mafunzo ya kuziba mapungufu aliyobainika kuwa nayo kabla ya kutunukiwa vyeti.

"Kupitia mpango huo mafundi waliojifunza kupitia sehemu za kazi sasa wanamudu kushindana kikamilifu katika soko la ajira kwa kuwa wametambua jinsi ya kufanya kazi zao kwa viwango vinavyohitajika kwenye soko," alisema Dk. Bujulu.

Alisema kuwa hatua hiyo imefanikiwa kutokana na VETA kuwa na ubunifu katika kutoa mafunzo ikiwamo kutoa mafunzo ya ujasiriamali na uanagenzi pamoja na mafunzo kwa njia ya simu (VSOMO) na hayo ya RPL.

Dk. Bujulu alibainisha kuwa kwenye vyuo vya VETA na vinavyosimamiwa na mamlaka hiyo wanatoa kozi 80 katika sekta 13, wameendelea na juhudi za kuhakikisha kila mkoa unakuwa na chuo ili kuwezesha wajuzi katika fani mbalimbali wanapatikana kwa maendeleo ya viwanda na taifa kwa ujumla.

"Ufundi stadi ni mkombozi mkubwa katika kukabiliana na tatizo la ajira, kwani ujuzi wa ufundi stadi unampa mhitimu fursa ya kuajiriwa na kujiajiri na hata kuajiri wengine," alisema.

Mwenyekiti wa DCPC, Irene Mark, alitumia nafasi hiyo kuwahamasisha waandishi wa habari kujiunga na kupata mafunzo ya kozi mbalimbali za ujasiriamali ili waweze kuyatumia katika kujiongezea kipato.

Awali Ofisa Mawasiliano wa VETA, Dora Tesha, alitaja baadhi ya kozi zinazotolewa na vyuo vyao kuwa ni pamoja na ufundi mchundo, ujenzi, magari, umeme wa viwandani na makazi, ushonaji, upambaji na urembo.

# CHINA: Tuheshimiane, tusiingilie masuala ndani ya nchi nyingine

**Na Mwandishi Wetu**

CHINA imetoa wito kwa mataifa mengine duniani kuheshimiana na kuacha kuingilia masuala ya ndani ya nchi nyingine kwa kisingizio chochote na kueleza kuridhishwa na namna mchakato wa uchaguzi mkuu unavyoendelea nchini.

Kauli hiyo imetolewa na Balozi wa China nchini, Wang Ke, jijini Dar es Salaam wakati wa mazungumzo na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge na kuongeza kuwa ni lazima mataifa yote yaendeleze uhusiano mwema miongoni mwao na kutoingilia masuala ya ndani ya mataifa mengine.

**Ni vyema mataifa yote yakaendeleza mahusiano mema miongoni mwao na kuhakikisha kuwa hayaingilii masuala ya ndani kati ya taifa moja na jingine.**

"Ni vyema mataifa yote yakaendeleza mahusiano mema miongoni mwao na kuhakikisha kuwa hayaingilii masuala ya ndani kati ya taifa moja na jingine," alisema Balozi Wang Ke.

Pia, alisema China itaendelea kuheshimu masuala ya ndani ya mataifa yote Tanzania ikiwamo na kueleza kuridhika kwake na mchakato wa kampeni za uchaguzi mkuu zinavyoendelea nchini na kuwatakia Watanzania kila la heri katika uchaguzi huo.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alisema ushirikiano baina ya Tanzania na China kisiasa, kiuchumi na kijamii ni madhubuti na imara na kwamba nchi yake itaendelea pia kuheshimu ushirikiano na mataifa mengine.

Aliishukuru China kwa ushirikiano wake wa kimkakati kwa Tanzania na kwamba utaendelea kudumishwa kwa maslahi ya pande zote mbili.

"Serikali ya Tanzania kwa kweli inaishukuru China kwa Ushirikiano wake wa kimkakati na tunakuahidi kwamba uhusiano wetu utaendelea kudumishwa kwa maslahi mapana ya pande zote mbili," alisema Balozi Ibuge.



Takataka zikiwa zimetupwa na kutelekezwa katika barabara ya Loyola, eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana, hivyo kuchafua mazingira. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Watoa huduma sekta gesi, mafuta waanza kunufaika

**Na Christina Mwakangale**

JUMUIYA ya watoa huduma ya sekta ya gesi na mafuta nchini (ATOGS), wataanza kunufaika na shughuli zao kwenye miradi mbalimbali baada ya kuingia makubaliano ya ukopeshwaji vifaa na fedha kutoka taasisi za kibenki.

Taasisi za fedha zilizoingia makubaliano na ATOGS ni Benki ya CRDB, Trade and Development Bank (TDB) pamoja na RentCo Africa.

Mwanzilishi na Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Abdulsamad Abdulrahim, akizungumza jana jijini Dar es Salaam baada ya makubaliano hayo, alisema lengo ni kuwawezesha Watanzania wazawa hususan makandarasi, wanaofanya kazi katika sekta hiyo kutekeleza shughuli zao kwa uhakika.

"Katika utafiti tulioufanya tulibaini, makandarasi wetu wana changamoto kubwa ya kukosa vifaa mfano magari ya kufanyia kazi kwenye miradi, ikiwamo buldoza na mashine mbalimbali.

Kuna fursa kwa wazawa katika miradi mikubwa hasa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), bomba la mafuta au mradi wa bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, sasa upatikanaji wa vifaa umekuja kufuta kilio cha Watanzania, tumepata mwarobaini, miradi mikubwa Watanzania watashiriki," alisema Abulrahim.

Alisema kampuni ya RentCo Africa, ambayo inafanya kazi katika nchi za Uganda, Rwanda, Kenya na Tanzania, itasaidia kuwapa mikopo ya vifaa wadau wa sekta hiyo, ili kuwawezesha kutekeleza kazi za miradi kulingana na kipindi cha mradi.

Alisema baada ya kukutana wadau hao walibaini kuna changamoto ya upatikanaji wa mikopo kwa wafanyabiashara ili kutekeleza miradi mbalimbali kutokana na masharti ya kibenki.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa RentCo Africa, Robert Nyasimi, alisema kampuni hiyo iliyo na makao makuu Kenya, inalenga kutoa mikopo ya vifaa ya na kwamba Watanzania wataweza kupata vifaa ili kutekeleza miradi mikubwa.

"Tunatarajia kuungana na benki, na taasisi mbalimbali zimesha kushirikiana nasi, CRDB wamekwishakubali, mikakati ni kukuza uchumi kwa nchi zetu," alisema Nyasimi.

Meneja Mwandamizi wa Mikopo ya Miradi Mikubwa kutoka Benki ya CRDB, Focus Mrosso, alisema benki hiyo tayari imeshatoa Sh. bilioni 30 kati ya Sh. bilioni 50, maalumu kwa ajili ya kusaidiwa wazawa kutekeleza miradi, ikiwamo SGR na bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere.

"Wazawa waliopata kazi, benki tunawapa mtaji ili waendeshe shughuli zote. Hawa ni makandarasi hata wauzaji vyakula katika miradi ili nao wafanye kazi," alisema Mrosso.

Mkurugenzi Mkuu wa TDB Kanda ya Afrika Mashariki, Lloyd Muposhi, alisema makandarasi wa nchi za Afrika katika miradi mikubwa wanashindwa kutekeleza miradi kutokana na changamoto za vifaa na fedha.

Alisema asilimia 80 ya mapato yanayotokana na miradi inayofanyika Afrika, inakwenda barani Ulaya kutokana na kutekelezwa na wageni.

# Mgombea CHADEMA kushinikiza wakulima wa korosho kulipwa

Na Thobias Mwanakatwe

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kyela kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alinanuswe Mwalwage, amesema akichaguliwa tu atakwenda kuweka kambi katika Ofisi ya Waziri wa Kilimo ili kuishinikiza serikali iwalipe fidia wakulima wa korosho wilayani Kyela ambao walichukuliwa mazao yao bila kulipwa.

Alitoa ahadi hiyo juzi baada ya kuelezwa na wananchi wa Kata ya Ngana kwamba walichukuliwa korosho zao mwaka jana na ilipofika Septemba mwaka huu wakarejeshewa na wengine bila kulipwa mauzo yao jambo ambalo limewaathiri kiuchumi.

**Suala la miundombinu ya barabara katika kata hiyo atalipatia kipaumbele ili kuhakikisha zinapitika muda wote.**

Kufuatia hali hiyo, Mwalwage aliwaahidi kuwa akichaguliwa tu atakwenda kuweka kambi kwa Waziri wa Kilimo ili kuhakikisha wakulima wote waliochukuliwa korosho kwa kuuza kwa mfumo wa ushirika uliosimamiwa na serikali wanalipwa fidia.

"Haiingii akilini kabisa unamchukulia mkulima korosho unakaa nazo mwaka mzima halafu unakuja kumrejeshea na humlipi chochote, huku ni kuendelea kumfanya mkulima aendelee kuwa maskini, kwenye ubunge wangu sitakubaliana na vitendo hivyo," alisema Mwalwage.

Mwalwage alisema sababu ya wakulima kukopwa mazao yao inatokana na serikali kutaka wakulima kuuza mazao yao kwa kutumia mfumo wa ushirika ambao vyama vya ushirika hununua mazao kwa kuwakopa.

"Hapa Kyela kuna Chama cha Ushirika Kyela (KCU) ndicho kilinunua korosho kwa wakulima kwa kuwakopa, cha kushangaza ilipofika Septemba na Oktoba wakulima walianza kurejeshewa korosho zao bila kulipwa fidia," alisema.

Aidha, Mwalwage alisema suala la miundombinu ya barabara katika kata hiyo atalipatia kipaumbele ili kuhakikisha zinapitika muda wote.



Mafundi wa kampuni ya Nyanza Road, wakijenga daraja la muda katika Mto Kerezange, eneo la Kitunda Kivule, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, baada ya la zamani kuharibika kutokana na mvua. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 200,000 kuondoka mpango wa kaya maskini

Na Elizabeth Zaya

ZAIDI ya kaya 200,000 zilizo chini ya mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) zinatarajia kutoka kwenye mpango kwa hiari baada ya maisha yao kuboreka zaidi na kutoka kwenye kundi lenye watu maskini zaidi.

Mkurugenzi wa Programu za Jamii kutoka TASAF, Amadeus Kamagenge, alisema mfuko huo umethibitisha kuwa idadi kubwa ya walengwa maisha yao yameboreka.

Kamagenge alisema kuwa tangu kuanza kwa mpango huo, umechangia kwa kiwango kikubwa katika kupunguza umaskini wa kipato katika kaya maskini nchini.

Kwa mujibu wa Kamagenge, mpango wa kunusuru kaya maskini kipindi cha pili cha awamu ya tatu kitahusisha kaya zote maskini nchini na kwamba lengo la mpango ni kuzipa nguvu zadi kaya hizo kujiongezea kipato na kuzisaidia kupata huduma za kijamii hususani chakula, elimu na afya.

Kamagenge alisema kaya zitakazojumuishwa katika kipindi hicho cha pili cha mpango ni 950,962 zilizo na watu wenye uwezo wa kufanya kazi na zenye watoto, kundi la pili ni kaya 185,345 zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi, lakini zisizo na watoto na kundi la tatu ni kaya 174,508 zenye wazee, wenye ulemavu na wagonjwa wa muda mrefu lakini zisizo ma watoto.

Alisema kundi la nne ni kaya 94,381 zenye wazee na watoto na kundi la tano ni kaya 1,958 ambazo ziko chini ya uongozi wa watoto na kwamba kwa ujumla kaya zote zitakazonufaika ni milioni 1.4.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema walengwa wa kipindi cha pili cha mpango huo watakuwa wanalipwa fedha zao kwa mfumo wa kielektroniki.

# TCU yafunga rasmi udahili vyuo vikuu

Na Christina Mwakangale

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imefunga rasmi udahili wa awamu ya pili kwa ngazi ya shahada ya kwanza, kwa mwaka wa masomo 2020/2021.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, waliokosa fursa ya kutuma maombi kwa awamu ya kwanza na pili, wasubiri maelekezo kutoka tume hiyo.

"Oktoba 18, mwaka huu, udahili wa ngazi ya shahada ya kwanza katika taasisi ya elimu ya juu. Hivi sasa vyuo vinaendelea kuchakata na kuidhinisha maombi ya udahili yaliyopokelewa vyuoni awamu ya pili," alisema Prof. Kihampa.

Alisema, mchakato wa kuidhinisha majina utakapokamilika, majina ya waliodahiliwa kwenye awamu ya pili yatatangazwa vyuoni Oktoba 24, mwaka huu.

Pia, Prof. Kihampa alisema muda wa kuidhinisha udahili kwa waliodahiliwa chuo zaidi ya kimoja kwa awamu ya kwanza, ulikamilika Oktoba 17, mwaka huu.

"Waombaji ambao bado hawajakamilisha uthibitisho wao, watapewa utaratibu mwingine wa kujithibitisha na hakuna mwombaji atakayekosa udahili kwa sababu ya kushindwa kujithibitisha," alisema Prof. Kihampa.

# 'Makundi maalum yapewe kipaumbele uchaguzi mkuu'

Na Christina Mwakangale

WAPIGAKURA wameshauriwa kutoa kipaumbele katika upigaji kura kwa watu wa makundi maalumu, ikiwamo walemavu, wazee na wajawazito.

Ofisa Elimu kwa Mpigakura kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Nuru Riwa, aliyasema hayo wakati akizungumza wa wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC).

Alisema jamii ikumbuke zimebaki siku chache, hivyo kila mpigakura atambue makundi hayo huku akiwataka waandishi kutoa habari zenye usahihi.

"Ikiwa zimebaki siku chache kuelekea uchaguzi mkuu, toeni kipaumbele kwa makundi maalumu, wazee, wajawazito, wenye ulemavu na hata kinamama waliobeba watoto," alisema Riwa na kuongeza:

Waandishi wa habari pia mnatakiwa kutangaza yanayostahili katika uchaguzi. Pia jamii ikumbuke kutovaa nguo zinazoonyesha au viashiria vya chama."

Alisema pia wapigakura wanaweza kuhakiki taarifa zao wenyewe kupitia simu zao za mkononi ili kufahamu vituo vya kupigia kura, kwa kupiga namba *152*00# kisha kufuata maelekezo.

Aidha, ikiwa zimebaki siku saba kuelekea uchaguzi mkuu, baadhi ya walemavu wameipongeza serikali kuandaa karatasi maalumu za kupigia kura kwa wenye ulemavu.

Josephat Igembe kutoka Taasisi ya Under the Same Sun, alisema hatua hiyo itasidia wenye ulemavu wa kuona na uoni hafifu.

Aidha, akiwashauri wagombea kutumia kipindi kifupi kilichobaki kuwakumbuka wenye ulemavu, kwa kuzingatia mazingira rafiki kwenye mikutano katika kampeni.

"Kipindi kilichobaki wenye ulemavu wawasikie angalau wagombea wanachokisema, wawaelewe.

Mfano sisi wenye ulemavu tunatakiwa tusikilize mkutano tukiwa kwenye kivuli," alisema Igembe.

Tanzania na rais mwanamke, taifa liko tayari kumpokea?

Ukurasa 12






Ukurasa 13

'Chonde chonde amani ya taifa haina mbadala'

siasa

JUMATANO OKTOBA 21, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

NYERERE 1922 -1999

# Mleta uhuru pekee hotuba zake zinasikika, kuvuta wengi hata leo

**Na Ani Jozeni**

KATI ya viongozi wa nchi za Afrika waliofikisha nchi zao kwenye uhuru wanaweza kutofautishwa kwa sifa mbalimbali.

Sifa hizo ni pamoja na kudumu kwa muda mrefu madarakani bila kujenga chuki zinazosababisha kuondolewa ikulu kwa mfano, kupinduliwa na jeshi linaloingilia kati kama ilivyokuwa wakati ule.

Nyingine ni kukabidhi mamlaka ya nchi kwa mtu mwingine kwa ridhaa yake na kuwaongoza wananchi kuonyesha utii kwake baada ya miaka mingi ya utawala wa mtu mmoja jambo alilolifanya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, na mwisho ni sifa nyingine ni usomi unaoitangaza nchi mbele ya dunia, sifa nyingine ya Nyerere.

Baadhi ya marais wa kwanza wa Afrika waliokuwa na mwelekeo wa fikra kama wa Mwalimu Julius Nyerere ni Dk. Kwame Nkrumah wa Ghana, hata hivyo aliondolewa madarakani.

Patrice Lumumba wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo alikuwa kiongozi aliyeleta hisia chanya za kupigania nchi, kuondoa migawanyiko ya kikabila na dhuluma ziwe ni za jadi au zinazotokana na ukoloni.

Aidha, pia alikwamishwa na nguvu za jadi zikishirikiana na zile za ukoloni, kupitia maslahi ya machifu na jeshi na mwisho aliangamizwa.

Wako waliodumu muda mrefu hadi kipindi cha kufikia uchaguzi wa vyama vingi vya siasa, akiwamo Dk. Kenneth Kaunda wa Zambia, ambaye kwa jumla aliongoza nchi kwa amani licha ya kukosana na makamu wake Simon Kapwepwe miaka iliyofuata.

Ilipofikia wakati wa vyama vingi hakutaka kuingia katika mzozo kwa kutoa madaraka kwa mtu mwingine naye aonyeshe utii kwake, ila akawa na imani na demokrasia, akagombea kama mgombea wa chama tawala, lakini akaanguka.



Kati ya marais waliofikia miaka mingi madarakani wengi walifia madarakani ndiyo nchi zao zikapata viongozi wengine, kwa mfano Jomo Kenyatta, Felix Houphouet-Boigny wa Ivory Coast, Ahmad Sekou-Toure wa Guinea aliyekuwa rafiki wa karibu wa Nkrumah na Nyerere.

Wako walioingia madarakani baadaye kwa mtutu wa bunduki, lakini wakafikia sifa ya waanzilishi wa taifa jipya, na mitihani hiyo imewakuta vile vile, kwani kati yao kuna Mobutu Seseseko ambaye alifia ugenini huku nchi ikiwa imeparaganyika, halafu Kanali Muammar Gaddafi ambaye upande mmoja wa nchi ulimuasi. Alipojaribu kuuzima uasi huo mabeberu waliingilia kati na kumuua.

Ila kuna upande mwingine wa mijadala ya kisomi ambako Mwalimu Nyerere alikuwa siyo mshindani wa yeyote katika Afrika, katika masuala ya uhusiano kibiashara kati ya nchi tajiri na nchi maskini.

Nyerere ndiye alikuwa msemaji wa nchi maskini kwanza kutokana na umahiri wake wa kidiplomasia, akiwa anakutanisha vyama vya ukombozi na wajumbe wa nchi za Magharibi, hasa Uingereza na Marekani.

Suala la msingi halikuwa ni uwezo kidiplomasia ila maadili ya heshima ya Mwafrika dhidi ya mfumo wa ubaguzi wa rangi Afrika Kusini, utawala wa Wazungu au walowezi wachache Zimbabwe, ukoloni mkongwe wa Ureno na mfumo mbaya wa kiuchumi duniani.

Aidha, alitofautiana na uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) kuhusu majanga ndani ya bara hili, akiangalia matukio kwa maadili halisi, utu wa binadamu, na siyo kutoingilia mambo ya ndani.

Katika suala la uhusiano wa nchi maskini na tajiri, Nyerere alikuwa kama nabii ambaye utukufu wake ulifikia kilele wakati akiaga dunia mwaka 1999.

Mwalimu alikuwa ametoa hisia kwa miaka mingi, hasa kuanzia mwaka 1981 wakati Tanzania ikisukumwa kuachana na ujamaa na kuiachia sekta binafsi ndiyo ifanye kazi.

Mijadala ilikuwa mikali wana CCM wengi walikuwa wanaamini kuwa taifa likiacha ujamaa si muda mrefu litakuwa limegawanyika likiwa na mabilionea dhidi ya hohehahe iwapo dola itaachia njia kuu za uchumi ziingizwe kwenye mikono ya watu binafsi. Hapa Afrika sauti ya Nyerere ilipaa zaidi.

Wakati huo mwaka 1981, Nyerere alianzisha usemi, 'the IMF is not an international ministry of finance,' kuwa ni mfuko wa kusaidia nchi, si wizara ya fedha ya kimataifa ya kuamua ni sera zipi za kufuatwa.

Miaka 18 baadaye msemo ulikuwa moja ya vianzio vya wimbi la 'Occupy' ambalo lilileta rabsha kokote bodi ya Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia walienda kukutana.

Suala lilikuwa ni kwamba mikutano hiyo ni kuwekana sawa kati ya wakubwa na kubana nchi maskini zilipe madeni kandamizi, ikafikia kujiuzulu mkurugenzi mtendaji wa IMF wakati huo, Michel Camdessus.

Ni mizania chanya ya madeni na mageuzi, kuwa hazitumbukii tena katika mkasa wa kukwama kulipa deni.

Kwa hiyo, hata baada ya miaka 21 ya kuondoka kwake hotuba zake, maono, michango yake, maelezo na kile alichozungumza wakati wa uhai wake yanapendwa, kuvutia wengi na bado kuna mengi ya kujifunza.

Unabii wa Nyerere kila unapozungumzwa kuna jambo la kujifunza.

# Tanzania na rais mwanamke, taifa liko tayari kumpokea?

Na Christina Mwakangale

KWA nchi za Afrika, marais wanawake wameshuhudiwa Liberia, Malawi, Uganda na Tanzania.

Ellen Johnson Sirleaf, ni kiongozi wa kwanza mwanamama Afrika akiwa Rais wa Liberia, aidha, yupo Joyce Banda, aliyekuwa Rais wa Malawi kuanzia 2012 hadi 2014, wakati Specioza Kazibwe, alikuwa Makamu wa Rais wa Uganda kuanzia 1994 hadi 2003.

Huyu aliandika historia Afrika kwa kuwa mwanamama wa kwanza kuongoza dola akishika nafasi hiyo barani humo. Tanzania haijaachwa nyuma Makamu wa Rais ni Samia Suluhu Hassan, anashika usukuni.

Kwa miaka takriban 60 ya uhuru wa Afrika kuwa na rais mwanamke kuliongoza taifa ni jambo nadra na hii inatokana na sababu mbalimbali ikiwamo dhana, mila na desturi za Kiafrika kuwa mwanamke hawezi kushika nafasi ya uongozi.

Mfumo dume, unatajwa kuwa chanzo ingawa kuna harakati mbalimbali za kukabiliana nao.

Sirleaf aliiongoza Liberia kwa miaka 12, licha ya uongozi wake kujawa na minong'ono pamoja na kashfa mbalimbali.

Mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini kuanzia miaka ya 1990 pamoja na mkutano wa dunia wa wanawake, huko Beijing China ulileta mapinduzi ya kijinsia na kiuongozi na wanawake wakaanza kuonekana kwenye taasisi mbalimbali pamoja na bungeni.

Balozi Getrude Mongella, alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, mwenye jukumu la kusimamia mkutano huo, alihamasisha wanawake kutoka Tanzania kwenda kushiriki kongamano hilo kubwa lililotia fora duniani.

Kwa mara nyingine uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Jumatano ijayo unahusisha wagombea 17 wa urais, wakiwamo wanawake wawili Queen Sendinga wa Alliance for Democratic Change (ADC) na Cecilia Mwanga kutoka Demokrasia Makini.

Uchaguzi huu ni mara ya pili kuwa na mgombea mwanamke katika kiti hicho, baada ya mwaka 2015, Anna Mghwira kugombea urais, kupitia Chama cha ACT-Wazalendo.

**VIONGOZI WANAWAKE NCHINI**

Dhana iliyopo miongoni mwa jamii kwamba, mwanamke hawezi kuwa kiongozi mkuu wa nchi, inaweza kuondolewa baada ya viongozi hao kupewa nafasi na kuonekana wanavyotekeleza majukumu yao.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan ni kiongozi aliyeshika nafasi ya juu ya uongozi wa nchi na ameonyesha kumudu nafasi hiyo lakini walikuwapo wengine walioshika nafasi za mbalimbali za uongozi, ikiwamo mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya.

Anne Makinda, Spika mstaafu wa Bunge ni kati ya wanawake walioshika nafasi za juu katika mhimili wa pili wa nchi na kuonyesha uwezo wa mwanamke.

Mbali na hao yupo Asha-Rose Migiro, aliyewahi kuwa Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa (UN) pamoja na Profesa Anna Tibaijuka, aliyeongoza Shirika la Makazi Duniani (UN HABITAT).



Balozi Dk. Asha-Rose Migiro, ni miongoni mwa wanawake viongozi mashuhuri duniani, amewahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Ellen Sirleaf wa Liberia ni rais wa kwanza mwanamama barani Afrika.

**KIKWAZO NI NINI?**

Kabla na baada ya uhuru inakadiriwa kulikuwa na idadi ndogo ya wanawake, wasomi kutokana na mila, desturi kwenye maeneo kadhaa na kufanya elimu kwa mtoto wakike isiwe muhimu kipindi hicho.

Makinda, ambaye alikuwa spika wa kwanza mwanamke, akizungumza kwenye moja ya mikutano iliyokutanisha wanawake, Septemba mwaka huu, anasema wanawake wengi hawana uthubutu na baadhi hukata tamaa kabla ya kufanya jambo.

Akiwa kwenye mkutano wa Baraza Kuu la Wanawake Vijana wa Kikristo Tanzania (YWCA), anasema zipo mila na desturi ambazo hazihitaji kurithiwa, ili mwanamke ajikomboe.

"Ukishakwenda kugombea huko ndiko unakutana na matusi na wanawake wengi waliogopa, wanafikiri hapana sababu. Vitu hivi lazima tupambane navyo, inatakuwa tusirithi mila na desturi zile. Ukishajua kwamba hapa wanakubagua na wewe unakwenda na njia zako, watoto wetu wa sasa ndio watakaonufaika," anasema Makinda.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), Joyce Shebe, anasema ana imani kuwa mifumo ya vyama vya siasa ikibadilika, mwanamke ataweza kufikia nafasi ya urais,

"Naamini kama Watanzania wapo tayari kumpokea rais mwanamke, wajue kuwa mwanamke hawezi kupatikana tukilala na kuamka asubuhi basi akapatikana yanahitajika maandilizi na kuungwa mkono," anasema Shebe.

> "Katika uchifu mwanamke inakuwa ni shida hapo zamani. Siku hizi mambo yameboreshwa, tunaye chifu mmoja mwanamke yuko Mbalizi.

**DESTURI NA JAMII**

Mzee wa mila wa jamii za Wasafwa wa jijini Mbeya, Chifu Mwashinga Roketi, anasema mabadiliko mengi yamefanywa na hivyo wanawake wanaweza kushika nyadhifa tofauti.

"Katika uchifu mwanamke inakuwa ni shida hapo zamani. Siku hizi mambo yameboreshwa, tunaye chifu mmoja mwanamke yuko Mbalizi.

Anasema Tanzania kuwa na rais mwanamke inawezekana, licha ya kwamba hapo awali hakuweza kusimama mbele ya mwanaume kwa sababu anakuwa katika 'siku zake' kwamba anakuwa hayupo katika usafi na hiyo ilikuwa zamani.

Mkazi wa Gongo la Mboto, Dar es Salaam Nestory Mwawa anasema kipindi cha mwanamke kuwa rais kinategemeana na jamii iwapo itamkubali, lakini anaona kuwa hana ujasiri na anategemea zaidi wanaume.

**WAGOMBEA URAIS**

Mgombea urais, Queen Sendega ambaye ni Naibu Katibu Mkuu ADC Tanzania Bara, anasema atafanya mabadiliko ya kiuchumi kwa miaka mitano iwapo atachaguliwa akilenga kuongeza ajira.

Mgombea huyu pia aliwahi kugombea ubunge Jimbo la Kawe mwaka 2015 kwa tiketi ya chama hicho, anasema ana stashahada ya biashara, huku akijishughulisha na masuala ya ujasiriamali na kilimo.

Aidha, ahadi zake katika kampeni ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanakombolewa na walio kwenye kipato cha chini katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza ya utawala wake, atatengeneza ajira milioni 10 licha ya kwamba hakusema atazitengeneza je.

Cecilia Mwanga ambaye ni mgombea wa Chama cha Demokrasia Makini chama ambacho kilisajiliwa mwaka 2001. Katika uchaguzi wa mwaka huu, anasema sera yao ni kusisitiza juu ya kilimo kwani ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania.

Mwanga anaahidi kuwa atafanya kampeni zake kwa kutumia usafiri unaotumika sana vijijini, kama baiskeli na Guta na atazingatia afya pamoja na amani kwa Watanzania.

**MTIZAMO WA JAMII**

Katika uchaguzi kuna dhana nyingi ambazo zinatajwa kwamba, wanawake wagombea hawapati muda wa kujiandaa au kuandaliwa kuwania nafasi za uongozi.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Bertha Koda, akizungumzia suala hilo, anasema mbali na changamoto zinazowakumba wanawake hao ndiyo hushiriki zaidi katika hatua nne za mchakato wa uchaguzi, ikiwamo kabla ya uchaguzi, kupiga kura, kuzihesabu, kutoa matokeo na baada ya uchaguzi kushangilia.

Prof. Koda akiwasilisha mada kuhusu haki za wanawake katika mchakato wa uchaguzi kwenye mkutano wa wanawake na viongozi jijini Dodoma, anasema takwimu zinabainisha kuwa asilimia 53 ya wapigakura uchaguzi mkuu mwaka 2015, walikuwa wanawake.

Aidha, anasema ongezeko la wanawake wapigakura kati ya waliojiandikisha mwaka 2015, linatokana na wadau na wanawake wenyewe kutambua kuwa kura ya mwanamke ni turufu ya ushindi.

# ‘Chonde chonde amani ya taifa haina mbadala’




Vijana ni wahamasishaji na washiriki wakuu wa uchaguzi kuanzia kampeni hadi kushangilia matokeo, watumie nafasi hiyo kudumisha amani na kuendeleza utulivu wa taifa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

KAMPENI za uchaguzi mkuu, sasa zameingia ngwe ya lala salama, zikiwa zimebakia siku saba ili kufikia Jumatano ijayo Oktoba 28 siku ya kupiga kura.

Jana Tume ya Uchaguzi (NEC) imeruhusu wananchi kutumia vitambulisho vya taifa, hati ya kusafiria na leseni kupiga kura kwa wale ambao watakuwa wamepoteza kadi zao.

Jumatano ijayo Watanzania wanakwenda katika vituo vya kupigia kura kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo hadi kufikia 2025, si jambo la kupuuza.

Kuanzia leo zinasalia siku saba za kampeni za uchaguzi huo wa nafasi ya urais, ubunge na udiwani kwa Tanzania Bara wakati Zanzibar wanamchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Zanzibar, wabunge na wawakilishi. Kampeni zitahitimishwa Oktoba 27, kisha itakuwa ni zamu ya wapigakura kufanya maamuzi.

Wagombea hao kutoka vyama vilivyojitosa katika uchaguzi huo, wanapoendelea kujinadi kwa wapigakura kwenye mikoa mbalimbali nchini, ili hatimaye wachaguliwe ama watoswe siku ya uchaguzi, wakumbuke kuwa wananchi wana wajibu wao na taifa lina haki ya kubaki na amani.

Wakati kampeni hizo zikiendelea, ni vyema wadau wa siasa kwa pamoja wakaongeza kasi ya kuhimiza amani bila kuchoka kipindi hiki, ili yote yanayoendelea yahitimishwe vizuri kwa utulivu.

Yamesikika matukio ya baadhi ya watu kuuliwa, wanafamilia wa wanasiasa kushambuliwa kwa risasa na watu kushambuliwa huko visiwani Pemba.

Kila mmoja ni muhimu akatambua kuwa baada ya hekaheka zote zinazoendelea, ni lazima maisha yaendelee, tena kuna awamu nyingine na mipango mingi baada ya uchaguzi.

“Wagombea wanatakiwa kuwashawishi wapigakura wenye sifa ya kupiga kura ili siku ikifika wafanye maamuzi yao kwenye sanduku la kura kuchagua viongozi tena kwa kutumia vitambulisho mbadala vilivyotangazwa na NEC kwa utulivu.

Hivyo wadau wa siasa kuanzia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, vyama vya siasa, viongozi wake, wanachama, wapigakura na viongozi wa dini kila mmoja afanye kazi yake.

Amani ni muhimu wakati huu wa kampeni na hata kwenye uchaguzi mkuu, kwa sababu bila amani inawezekana watu wasijitokeze kushiriki katika uchaguzi huo, hivyo ni vyema iwe amani kwanza mengine baadaye.

Suala hilo ni la msingi kwa kuwa kumekuwapo na taarifa za baadhi ya watu kuumizana wakati huu wa kampeni, hali ambayo inastahili kukemewa na wadau wote, ili jukumu hilo lifanyike kwa utulivu.

Amani ikiwapo Watanzania watajitokeza kuchagua viongozi wanaowataka, lakini vinginevyo wanaweza kuhofia usalama wao wakaacha kwenda kupiga kura vituoni Jumatano ijayo Oktoba 28.

Vilevile hatua ya kuhimiza amani umoja na mshikamani vilivyopo nchini ni muhimu ili Watanzania waendelee shughuli zao kwa uhuru bila vurugu na kujiletea maendeleo, kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Ikumbukwe kuwa, kuvunja amani kunaweza kuwa kazi rahisi, lakini kuirudisha ni vigumu kupindukia, hivyo wadau wa siasa na wapigakura washiriki kikamilifu katika jambo hili kwa kuwahimiza wanasiasa kutambua tunu hiyo iliopo nchini.

Si vibaya kuwaambia wanasiasa kuwa wawe makini katika kampeni zao kwa kuepuka kutoa lugha za matusi, kuudhi na badala yake wajikite katika kutangaza ilani za sera zao, ili kushawishi wapigakura wawachague.

Ni wazi kuwa wagombea wanaweza kuchaguliwa bila kutukuna ama kutumia lugha mbaya dhidi ya wenzao, wanachama wa vyama vingine, kwa kuwa kwenda kinyume na hayo ni sawa na kuamsha hasira za watu na kusababisha amani ivurugike.

Suala la kuhimiza utulivu linatakiwa liende pamoja na kutenda haki na haki iwe tunda la amani na yote yawe kama wimbo vinywani mwa wadau wote wa siasa ili kubadili mtazamo wa wanasiasa ambao wanetegemea matusi ama lugha chafu kama mtaji dhidi ya wagombea wenzao waache.

Wagombea wanatakiwa kuwashawishi wapigakura wenye sifa ya kupiga kura ili siku ikifika wafanye maamuzi yao kwenye sanduku la kura kuchagua viongozi tena kwa kutumia vitambulisho mbadala vilivyotangazwa na NEC kwa utulivu.

Utii wa sheria za uchaguzi bila shurutu kama vile siku ya uchaguzi kuacha kufanya kampeni, kutokuvaa fulana, kuwa na picha au nembo za mgombea au chama ni mambo ya kuzingatia.

Aidha, kupiga kura na kukaa nyumbani ni jambo jema kama inavyoelekezwa. Lakini kwa upande mwingine, vijana nao wanatakiwa kuwa makini na kukataa kutumiwa vibaya na wanasiasa, kama ambavyo Rais John Magufuli na mgombea wa CCM, anavyowatahadharisha kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi mkuu na wasikubali kutumiwa kuingia barabarani.

Anawaonya kuwa atasikitika kuona kuwa wananchi wanaumia baada ya uchaguzi mkuu.

Siyo vibaya vijana kuingia kwenye siasa, kwa kuwa ndiyo viongozi wa taifa kesho na wana nafasi ya kuandaliwa vyema kwenye ulingo wa siasa badala ya kutumika kufanya vurugu kwa manufaa ya wanasiasa.

Hivyo, wakati huu ambao Tanzania inaingia katika uchaguzi wa sita ndani ya mfumo wa vyama vingi, ni muhimu kuendelea kuweka amani na haki mbele, kutokana na kuwapo kwa taarifa za baadhi ya watu kuumizwa katika kampeni.

Taarifa za aina hiyo si dalili njema, ndiyo maana nguvu za pamoja za wadau wa siasa, zinahitajika kwa ajili ya kuhimiza amani, ili vijana ambao ndiyo wanaodaiwa kutumiwa vibaya na wanasiasa, waache kujeruhi badala yake wajenge taifa.

MIKHAIL GORBACHEV

# 'JEMBE' LILILOBWAGA UKOMUNISTI URUSI, KUMALIZA VITA BARIDI

## •Alichomoka Ikulu Krismasi



**Na Mwandishi Wetu**

MIKHAIL Gorbachev, (pichani) aliyezaliwa Machi 2, 1931 huko Privolye nchini Russia ambayo zamani ilikuwa ikijulikana kama U.S.S.R ameacha historia kwa kuibadilisha Urusi.

Ni mwanamageuzi alianza kazi ya kuondoa uhafidhina wa Kikomunisti akiwa ndani ya chama wakati huo, akiwa Katibu Mkuu wa Chama cha Kikomunisti cha Urusi (CPSU) kuanzia mwaka 1985 hadi 1991.

Aidha, alikuwa Rais wa Urusi kuanzia Machi 15, 1990 - hadi Desemba 25, 1991 ikiwa ni kiongozi aliyeishi Ikulu kwa miezi tisa na kuchomoka siku ya sikukuu ya Krismasi au Noel.

Juhudi za Gorbachev za kuifanya Urusi kuwa ya kidemokrasia zaidi na kuifanya nchi yenye uchumi wa soko huria ziliitumbukiza kwenye anguko la ukomunisti na kuvunjika kwa muungano wa Jamhuri za Kisovieti mwaka 1991.

Kabla ya anguko hilo la taifa kubwa lililokuwa kisikika kwenye vita baridi vilivyokuwa kati ya Urusi na Marekani, Gorbachev, alikuwa mshindi wa tuzo ya Amani ya Nobel mwaka 1990.

### ALIKOTOKA

Historia inaonyesha kuwa mwaka 1952 aliingia katika Chuo Kikuu cha Moscow State akisoma sheria alikohitimu mwaka 1955 na kuanza kuwa mwanachama wa Chama cha Kikomunisti cha Urusi (Communist Party), aliendelea hatua kwa hatua hadi kufikia wadhifa wa kuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti mwaka 1971.

Baada ya kifo cha Katibu Mkuu wa Chama cha Kikomunisti Yury Andropov, mwaka 1984 na Konstantin Chernenko kuwa mrithi wake, dalili zilionyesha kuwa Gorbachev angekuwa mrithi wa Chernenko, aliyefariki Machi 1985 na kazi ikamwangukia Gorbachev.

Gorbachev alianza uongozi wa chama akiwa na lengo la kuamsha kwa nguvu uchumi wa Urusi uliodumaa kwa kipindi chote cha Rais Leonid Brezhnev, kuanzia 1964 hadi 82.

Aliingia na mkakati wa kuleta mabadiliko ya kiteknolojia na kuboresha zaidi matumizi ya teknolojia, kiuchumi ilikuwa ni kuongeza uzalishaji kwa tija na kuufanya mfumo wa uongozi wa serikali kuwajibika na kufanyakazi kisasa.

### KUANZISHA UWAZI

Baada ya kuona mambo hayo yameshindikana na hayakuleta matokeo yenye tija Gorbachev kuanzia mwaka 1987 hadi 88 alianzisha mkakati mpya wa kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa akitangaza sera ya 'uwazi' au kwa Kirusi glasnost au "openness".

Uwazi ukayeyusha mambo mengi yaliyokuwa yameganda kwa mfano uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari haki hiyo ikapanuka, uhuru mwingi kwa vyombo vya habari na kuruhusu kukosoa serikali na kutoa maoni mbalimbali ukapewa enzi.

Ukiritimba wa chama kushika hatamu ulianza kupungua ukipambanuliwa katika sera ya Gorbachev ya perestroika (mageuzi). Chini ya uongozi huo wagombea wengi waliruhusiwa, kupiga kura ya siri kukaanza kupata viongozi wa chama na pia ukawa mwanzo wa kuwa na sera za soko huria kwenye uchumi.

### UHURU KIMATAIFA

Gorbachev tangu mwanzo alikuwa ameshatengeneza mazingira ya kiushirikiano na mataifa ya mashariki na magharibi na ilipofika Desemba 1987, alitiliana saini na aliyekuwa Rais wa Marekani Ronald Reagan kuteketeza makombora ya nyuklia na mwaka kati ya 1988 hadi 1989 Katibu Mkuu wa Chama Gorbachev, alisimamia kuondolewa kwa vikosi na majeshi ya Urusi huko Afghanistan, baada ya kuikalia nchi hiyo.

Gorbachev anaweza kuitwa jembe lililosimamia mabadiliko mengi nchini Urusi kuanzia mwaka 1989 hadi 1990 , ambayo yalikamilisha mageuzi kisiasa barani Ulaya na kuwa mwanzo wa kukomesha vita baridi duniani vilivyokuwa vikionyesha ukuu wa mataifa ya Marekani na Urusi.

Mwaka 1989 alitumia mbinu zote kuunga mkono mabadiliko kwenye ukomonisti lakini kwenye Jamhuri za Urusi za Ulaya Mashariki lakini zilipoanguka Gorbachev, aliunga mkono kimya kimya anguko lao.

Vuguvugu la uhuru na fikra za kuachana na Ukomunisti uliochagizwa na Gorbachev, lilisababisha vurumai za kisiasa na machafuko katika Jamhuri za Azerbaijan, Georgia na Uzbekistan zikitaka kuwa huru na kujitenge na urusi, mojawapo ni Lithuania, hata hivyo mambo yalidhibitiwa na uongozi wa Gorbachev huku marekebisho ya katiba yakifanyika ili kuzifanya nchi hizo kuwa na uhuru kamili na kujitenga na Jamhuri ya Urusi U.S.S.R.

### RAIS WA URUSI MPYA

Machi 1990 bunge lilimchagua kuwa Rais wa U.S.S.R akiwa na mamlaka yote na akaacha historia chini ya uongozi wake kwa kukifutia nguvu nyingi na madaraka Chama cha Kikomunisti, na kutoa uhuru wa kuwapo vyama vingi.

Hata hivyo, katika mazingira ya kuleta mabadiliko na kuunda Urusi mpya, uchumi uliyumba na kuanguka, watu wakiwa na hali ngumu kiuchumi, Gorbachev alihisi kuchanganyikiwa na kufungamana na wahafidhina wa chama hicho pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama.

Watetezi wa fikra za Ukomunisti na Urusi kwanza na wapinga mabadiliko na mageuzi walihakikisha Gorbachev, na familia yake wanawekwa kwenye kifungo cha ndani ya nyumba kuanzia Agosti 19 hadi 21 mwaka 1991 katika kile kinachoelezwa kuwa ni mapinduzi baridi yaliyodumu kwa muda mfupi yakiongozwa na wenye msimamo mkali.

Baada ya mapinduzi hayo mepesi, yaliyoongozwa na wapinga mageuzi akiwamo Boris Yeltsin na wengine licha ya Gorbachev kurudi ikulu baada ya kifungo cha nyumbani, alijiunga nao, lakini akaondoka kwenye Chama cha Kikomunisti.

Alivunja kamati kuu na kuondoa uwezo wa chama kulidhibiti Shirka la Ujasusi la the Urusi KGB na majeshi ya nchi hiyo. Na ilipofika Desemba 25, 1991, Gorbachev alijiuzulu uongozi wa USSR na ukawa mwisho wa muungano wa jamhuri za Kirusi na ikaanza kuitwa Russia.

### KUACHANA NA SIASA

Mwaka 1996 Gorbachev aligombea urais, lakini akaambulia patupu na ilipofika 2006 aliingia ubia na bilionea wa Kirusi na mwanasheria Aleksandr Lebedev, wakanunua gazeti la Novaya Gazeta, lililokuwa linapinga na kukosoa Ikulu ya Urusi maarufu kama Kremlin.

Wawili hao Septemba 2008 walitangazwa kuwa waanzisha chama cha kisiasa kinachomilikiwa na Gorbachev na Lebedev, hata hivyo hakikuonekana kwenye uwanja wa kisiasa. Licha ya kwamba Gorbachev alikuwa wakati mwingine mpinzani mkuu wa Rais wa Urusi Vladimir Putin, alionekana kuunga mkono baadhi ya masuala yanayotekelezwa na Putin.





# Maandalizi sensa ya watu, makazi yaanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imesema inaendelea na maandalizi ya sensa ya watu na makazi na itafanyika ndani ya kipindi cha serikali ya awamu ya tano.

Aidha, imezitaka taasisi za umma na sekta binafsi kutumia takwimu zinazozalishwa na ofisi hiyo ili kusaidia mipango mbalimbali ya nchi.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Takwimu Duniani yenye kauli mbiu 'Kuiunganisha Dunia kwa Takwimu Tunazoziamini'.

Alisema kamisheni ya takwimu Bara la Afrika imekubaliana nchi zote 54 zinatakiwa kufanya sensa hiyo na kwamba kwa Tanzania imeendelea na maandalizi yake ili kufanya sensa kwa muda uliopangwa.

Kadhalika, alisema licha ya Tanzania kuwa na mafanikio makubwa kwenye uimarishaji wa mifumo ya takwimu bado kuna tatizo la matumizi ya takwimu zinazozalishwa na ofisi hiyo kwa wadau wengine.

"Kuna dhana imejengeka kwamba takwimu zinazozalishwa ni za serikali hapana, takwimu zinatakiwa kutumika na kila mmoja, watu wengine wanaachwa nyuma, tumetoa takwimu tumetoa hali halisi, lazima mtu atafakari huu mfumuko wa bei atumie fursa ipi," alisema.

Aliongeza: "Maendeleo hayapangwi na mtu mmoja bali yanapangwa na kila mmoja wetu, tutumie takwimu kupanga maendeleo yetu, ndio maana hata ukitaka kwenda kununua vitu sokoni unaangalia kitu gani hakipo, pale ni unakusanya takwimu."

Alibainisha kuwa asilimia 100 ya takwimu wanazozalisha zinatumiwa na serikali.

"Tunashukuru serikali ya awamu ya tano kila kiongozi akisimama anazungumza takwimu, tambueni maendeleo hayaletwi na serikali pekee bali na kila mmoja wetu, sisi Ofisi ya Takwimu imeendelea kuboresha uwezo wa watakwimu katika wizara, idara na taasisi za serikali kupitia mpango wa kwanza wa kuboresha na kuimarisha takwimu nchini," alisema.

Aidha, alisema ofisi hiyo itaendelea kupunguza gharama za kufanya utafiti kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuondokana na mfumo wa kutumia karatasi.

"Tutaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu ya uzalishaji wa takwimu na kuendana na wakati, takwimu ni muhimu katika kupanga maendeleo ya watu," alisema.

Mtakwimu huyo alisema janga la corona limeongeza umuhimu wa data na takwimu na limeonyesha dunia kwa namna gani taarifa za kijiografia zinavyoweza kusaidia kufuatilia kasi ya mwenendo wa mabadiliko duniani.

Dk. Chuwa ambaye ni mwenyekiti kamisheni ya takwimu Afrika, alisema wamekubaliana kila nchi iandae mkakati wake ambao utatumika kuandaa dira ya maendeleo bara la Afrika ya mwaka 2020-2063.

Pia alisema wamekubaliana kuendeleza watakwimu ili kuwa na weledi.

# Watanzania waaswa kauli za wanasiasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kuwa makini na maneno ya wanasiasa ambayo yanaweza kuchafua sifa ya nchi kuwa kisiwa cha amani duniani, wakati huu ambao Taifa linaelekea kwenye uchaguzi mkuu wiki ijayo.

**Watanzania wanatakiwa kuwa makini na maneno ya uchochezi ya wanasiasa ili kuilinda amani iliyopo nchini.**

Mkurugenzi wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Ibrahimu Twaha Ibrahimu, alitoa wito huo juzi katika mahafali ya tano katika Shule ya Msingi ya Zamzam Islamic jijini Dodoma.

Alisema, Watanzania wanatakiwa kuwa makini na maneno ya uchochezi ya wanasiasa ili kuilinda amani iliyopo nchini.

"Watanzania maneno ya wanasiasa yasiwe chanzo cha sisi kufanya machafuko na kuiharibu amani yetu kwani mataifa mengi yamekuwa yakitamani kutuharibia amani yetu tuliyoilinda kwa muda mrefu sasa," alisema Ibrahim.

Aidha, alisema Watanzania wanatakiwa kuendelea kumwomba Mungu aliepushe Taifa na jicho la husda, ili uchaguzi mkuu 2020 wa madiwani, wabunge pamoja na Rais upite kwa salama na amani.

Akizungumzia masula ya elimu nchini, aliwataka Waislamu kote nchini kusomesha watoto wao katika shule bora ambazo pia zinawajengea watoto kwenye misingi bora ya kiimani.

Ibrahimu alisema kuna baadhi ya wazazi wanataka kuwasomesha watoto katika elimu ya dini pekee huku wakisahau kuwa wanatakiwa kuzalisha vijana watakaokuwa viongozi wazuri.

Kiongozi huyo pia alisema mpango wa kusomesha elimu ya dini ni mzuri, lakini katika kipindi cha sasa ni lazima mambo yote mawili yaende sambamba.

"Tunasisitiza somesheni watoto wenu na hata watoto wa kike nao wanatakiwa kusoma kwa bidii na kupata maarifa zaidi ili wasiangukie katika kundi la kuonewa katika jamii," alisema Ibrahimu.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Mohamed Bura, alisema pamoja na changamoto nyingi wanazopitia, lakini bado shule yao inaendelea kufanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani ya darasa la nne na la saba.

Katika risala iliyosomwa na mwanafunzi Aisha Ali, waliomba Taasisi ya Islamic Foundation kuwasaidia kumaliza ujenzi wa madarasa ambayo hayajakamilika kwa muda mrefu.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Haji Talib Mwinyi, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dodoma na Viwandani, kuhusu majukumu ya wizara hiyo, wakati akifungua semina ya elimu kwa umma, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Habari wa wizara hiyo, Emanuel Buhohela. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Watumishi ofisi ya wakili mkuu wahimizwa kuzingatia maadili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKILI Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, amewataka watendaji wa ofisi yake kufuata miiko na maadili ya kazi ili kutimiza wajibu wao ipasavyo.

Malata aliyasema hayo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo watendaji wa ofisi hiyo, iliyofanyika jijini hapa.

"Nawaagiza kuzingatia maadili na miiko ya kazi yenu naamini wote mtakuwa mnajua wajibu wenu, mnapaswa kufuata ili mtimize wajibu wenu kikamilifu," alisema.

Aidha, aliwataka kuwa wawajibikaji kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuitendea haki taaluma hiyo.

"Mawakili ni watu muhimu sana, lakini umuhimu wao unazidi kuonekana pale wanapofanya vitu ambavyo vinaleta matokeo chanya katika jamii," alisema.

Aliwataka mawakili kwenda kutekeleza kazi zao kiufasaha ili kuleta tija kwa jamii inayowazunguka.

"Tumieni kikamilifu pia mafunzo mliyoyapata katika kwenda kukabiliana na kesi za rushwa ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara...pia hakikisheni mnafanya kwa ufasaha namna ya uandaaji, hati za madai, maelezo ya mashahidi, stadi za utetezi na viapo vya maombi," alisema.

Alisema suala la rushwa lipo kila sehemu na kumekuwa na kesi za aina mbalimbali za rushwa katika vitengo tofauti.

Malata alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo mawakili hayo kufanya kwa ufanisi kesi zinazohusu rushwa.

"Mna kila sababu ya kujiamini, mnaweza kwa sababu mmejifunza vitu vya msingi ambavyo vinatumika katika kesi za kila siku," alisema.

Alieleza kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kwenda kutekeleza kwa vitendo yale aliyoyapata katika mafunzo.



# Matatani madai kumchoma moto mama wa kambo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu 10, wakiwamo vijana wawili wa familia moja kwa madai ya kumchoma moto mama yao wa kambo, wakimtuhumu kutumia hati ya nyumba zao za urithi kuchukua mkopo benki.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Oktoba 18, mwaka huu, saa 12:00 alfajiri kwenye Mtaa wa ZZK, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Aliwataja vijana hao kuwa ni Ezekia Lizer (20) na kaka yake Baraka Ezekia (24) ambao walimchoma moto mama yao wa kambo, Daines Mdee (26).

Kamanda Matei alisema awali, vijana hao walifiwa na mama yao na ndipo baba yao akamuoa Mdee na baadaye baba yao naye akafariki, hivyo wakabaki na Mdee na kwamba waliachiwa mali mbalimbali zikiwamo nyumba mbili.

**Tukio la pili linawahusu watu watano wakiwamo wanne wa familia moja ambao wanatuhumiwa kumuua baba yao kutokana na ugomvi wa mashamba.**

Alisema baadaye mama yao wa kambo alikwenda benki akachukua mkopo wenye thamani ya Sh. milioni 40 kuweka rehani nyumba zote mbili kisha akaenda kufungua duka, lakini akawa hapeleki marejesho benki.

"Baada ya muda benki wakaamua kuziuza nyumba hizo ili kufidia mkopo huo na ndipo vijana hao wakapandwa na hasira wakitaka kumuua. Walinunua petroli lita 10, lakini wakammwagia lita mbili kisha wakamchoma moto," alisema Kamanda Matei.

Alisema majirani walishtuka wakati mama huyo ameshawashwa moto lakini alikuwa tayari ameshaungua zaidi ya asilimia 80 ya mwili wake na ndipo walipoamua kumpeleka katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa ajili ya matibabu.

Matei alisema upelelezi wa shauri hilo unaendelea na ukikamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Kamanda Matei alisema tukio la pili linawahusu watu watano wakiwamo wanne wa familia moja ambao wanatuhumiwa kumuua baba yao kutokana na ugomvi wa mashamba.

Aliwataja watu hao kuwa ni Idrisa Mzinge (24), Jumanne Mazinge (30), Fikiri Rasi (38) na mama yao mzazi Chausiku Mahamudu (50) wakazi wa Kitongoji cha Mbuyuni wilayani Mbarali ambao wanatuhumiwa kupanga njama ya kumuua baba yao, Ali Mazinge (66).

Alisema tukio hilo lilitokea Juni 25 mwaka huu, ambapo wana familia hao walimkodi mtu mmoja kwa dau la Sh. 700,000 ili awasaidie kumuua baba yao na ndipo wakafanikisha tukio hilo.

Tukio la mwisho, alisema linawahusu wafanyabiashara ni Gorden Kidumba (23) na Mario Wikesi (20) ambao wote ni wakazi wa Ilembula mkoani Njombe wanaotuhumiwa kuiba pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji).



Wananchi wakishuhudia mzozo kati ya dereva wa daladala na bajaji, baada ya vyombo vyao kukwaruzana katika kituo cha mabasi cha Kabwe jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Saratani macho kwa watoto yashamiri

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UGONJWA wa saratani ya macho kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, umeanza kushamiri mkoani Mbeya, imeelezwa.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho katika Hospitali ya Rufani Mbeya, Dk. Fariji Kilewa, alisema kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, watoto 23 wenye umri wa kati ya miaka sifuri hadi mitano, wamebainika kuugua ugonjwa huo.

Alisema tatizo hilo linazidi kuwa kubwa kutokana na wazazi wengi kutojua dalili, hivyo kushindwa kuchukua hatua za haraka kuzuia au kutibu ugonjwa huo kwa watoto wanaougua.

"Katika kipindi cha kuanzia 2015 hadi Septemba, mwaka huu, tumebaini watoto 23 ambao tayari wamepata maambukizi ya ugonjwa huu. Hali hii si nzuri ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo watoto wanaokutwa na ugonjwa hu ilikuwa ni nadra sana kuwapata," alisema Dk. Fariji.

Kuhusu chanzo cha ugonjwa huo, Dk. Fariji alisema miongoni mwa sababu za watoto kuugua saratani ya macho ni pamoja na mabadiliko ya vinasaba vya wazazi.

Alisema ili kuepuka watoto kuugua ugonjwa huo, ni vyema kabla ya watu kufunga ndoa, kila mwanandoa akafahamu historia ya mwenzake kama ndani ya familia zao hawajahi kuathiriwa na ugonjwa huo ili kuchukua tahadhari ya watoto watakaozaliwa.

Dk. Farij alisema punde tu mtoto anapozaliwa anaweza kuhisiwa kuwa ataugua saratani ya macho endapo ataonekana macho yake yanang'aa nyakati za usiku kama yalivyo macho ya paka.

Alisema wazazi wanapoona dalili hiyo, wanapaswa kuchukua hatua ya kumpeleka mtoto hospitalini ili afanyiwe uchunguzi na kuchukua hatua za kuudhibiti kabla madhara hayajawa makubwa.

Alisema endapo hatua hazitachukuliwa haraka, utatokea uvimbe ndani ya jicho lenye dalili hizo na uvimbe huo utasambaa mwili mzima na itafikia hatua ambayo kutakuwa hakuna tena tiba na mtoto huyo atapoteza maisha.

# Mgombea CUF ajinadi kujali wafanyabiashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Raphael Ngonde, amesema endapo atachaguliwa, atahakikisha wafanyabiashara wanawekewa mazingira rafiki ya kufanyia shughuli zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ngonde alisema atahakikisha anawapigania wafanyabiashara ili Sheria ya Kodi ya mwaka 2016 hasa kipengele cha ukadiriaji wa kodi, kirekebishwe kwa maelezo kuwa kinatumika kuwanyanyasa.

Ngonde alisema hata wafanyabiashara wadogo, maarufu kwa jina la machinga, wanafanya shughuli zao katika mazingira magumu liche ya kupatiwa vitambulisho vya wajasiriamali wanavyopewa na rais.

Ngonde alisema wajasiriamali wengi wanauza bidhaa zao kwa kupanga chini hali ambayo inazifanya zikose thamani hasa katika kipindi hiki ambacho taifa limeingia kwenye uchumi wa kati.

"Tunatakiwa tuweke mazingira rafiki kwa ajili ya wafanyabiashara wetu, hapa kwetu Mbeya tuna wafanyabiashara wengi ambao wanafanya shughuli zao kwenye mazingira magumu, sasa nawaomba wanichaguwe ili nikahakikishe tunabadilisha sheria za kodi," alisema Ngonde.

Alisema amekuwa akifanya kampeni zake kwenye maeneo mbalimbali ya jimbo na amekuwa akikusanya kero za wananchi ambazo ataenda kuziwasilisha bungeni endapo atachaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo.

Ngonde alisema mikutano yake ya kampeni imekuwa ikijaa wananchi ambao ni wanachama wa vyama vyote vya siasa na wamemwahidi kumpigia kura kutokana na sera zake.

Alisema kwa sasa jimbo hilo linahitaji mwanasiasa kijana ambaye ni yeye na kwamba atahakikisha analibadili jiji hilo na kulifanya liwe linang'aa.

**Mikutano yake ya kampeni imekuwa ikijaa wananchi ambao ni wanachama wa vyama vyote vya siasa na wamemwahidi kumpigia kura kutokana na sera zake.**



# Shein aaga akijivunia mafanikio miaka 10

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewaaga wananchi kwa kumaliza miaka 10 ya kuiongoza Zanzibar na kuwaambia kuwa awamu ya saba imefanya mambo mengi na anawaachia amani na utulivu.

Dk. Shein aliyasema hayo jana katika viwanja vya Mao Dze Dong, Zanzibar katika hotuba yake ya kuwaaga wananchi wa mikoa mitano ya Zanzibar pamoja na kuzindua Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050.

Alisema mbali na jitihada alizochukua za kuwaachia wananchi mifumo na vitu ambavyo vitarahisisha mwenendo wao wa kujipatia huduma za maisha, pia vile anawaachia zawadi ya amani na utulivu.

Kutokana na amani hiyo, aliwasihi wananchi kuzidisha upendo, umoja na mshikamano miongoni mwao ili zawadi hiyo anayowaachia idumu na kung'ara zaidi.

"Zawadi hii ya amani na utulivu mtaitumia ninyi na vizazi vitakavyokuja baadaye kwa hivyo itunzeni sana na muilinde kwa nguvu zenu nyote," alisema Dk. Shein.

Pia alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, awamu ya saba bila kutetereka, kinyume cha matarajia ya wale waliokuwa hawaitakii mema, imefanya mambo mengi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Alitanabahisha kuwa serikali imetekeleza mambo ya maendeleo kwa kuzingatia shida na kero mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili wananchi kwenye huduma za msingi za jamii.

Aliongeza kuwa wananchi wamekuwa wasikivu katika kufuata taratibu na sheria za nchi mambo ambayo taasisi zilizopewa majukumu ya ukusanyaji wa mapato kufanya vizuri.

Dk. Shein alisma wananchi wa Zanzibar wanathamini jitihada zilizochukuliwa na serikali yao katika kuleta maendeleo na kuziunga mkono jitihada hizo katika kuleta maendeleo yenye ufanisi ambayo wanajivunia.

Kuhusu Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, alisema maandalizi yake yamezingatia mabadiliko ya haraka ya sayansi na teknolojia duniani, fursa zinazojitokeza katika sekta zinazoibua zikiwamo uchumi wa kutumia rasilimali za bahari (uchumi wa bluu, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), mafuta na gesi asilia.

**Wananchi wamekuwa wasikivu katika kufuata taratibu na sheria za nchi mambo ambayo taasisi zilizopewa majukumu ya ukusanyaji wa mapato kufanya vizuri.**

# Samia ataka Watanzania kulinda uhuru wa nchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Samia Suluhu Hassan, amewataka wananchi kulinda uhuru wa nchi, Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanzania ambao umechangia kukuza uchumi wa nchi.

Akizungumza juzi katika mkutano wa kampeni Paje, Kusini Unguja, alisema CCM imeleta utawala bora na utawala wa sheria ili wananchi wafanye shughuli zao za kiuchumi bila bugudha.

Samia alisema CCM haijafanya makosa kumchagua Dk. Hussein Mwinyi kuwa mgombea urais wa Zanzibar kwa sababu ni mtu mwadilifu na mchapakazi hodari ambaye anaweza kuiongoza nchi.

"Wana CCM tushikane, twende tukapige kura na tulichague jembe letu Dk. Mwinyi kwa Zanzibar na Dk. (John) Magufuli kwa Tanzania Bara na wagombea wote wa CCM," alisema Samia.

**Kuna uchakavu wa majengo ya shule na uhaba wa walimu katika Mkoa wa Kusini Unguja, hivyo akiwa Rais atawekeza katika elimu ili wananchi kupata elimu bora.**

Alisema mgombea huyo anafanya kampeni nzuri za kuwafikia wananchi popote walipo na kusikiliza matatizo yao ili akipata urais ayafanyie kazi.

Serikali, alisema imejipanga kuhakikisha siku ya uchaguzi kunakuwa na amani ili wananchi waende kupiga kura bila uvunjifu wa amani na kuwatahadharisha wananchi kutouza vitambulisho vya kupigia kura kwa sababu kufanya hivyo ni sawa na kuuza utu wao.

Naye Dk. Mwinyi alisema kuna uchakavu wa majengo ya shule na uhaba wa walimu katika Mkoa wa Kusini Unguja, hivyo akiwa Rais atawekeza katika elimu ili wananchi kupata elimu bora.

Alisema anafahamu kuwa kuna uhaba wa wahudumu na wataalamu wa afya, hivyo atawekeza huduma hiyo na kuongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba ili wananchi wapate huduma za afya bora.

Kuhusu huduma ya majisafi na salama ataweka miundombinu hiyo ili wananchi wapate majisafi na salama.

Alisema atairasimisha Bandari ya Kizimkazi ili itoe huduma bora kwa wananchi wa kusini.

Pia alisema atawawezesha wakulima wa mwani ili bei ya zao hilo kuwa nzuri na wakulima kunufaika na kilimo hicho.

Sambamba na hilo, alisema atahakikisha kila eneo lenye uwekezaji wa utalii atahakikisha vijana wapate ajira ili utalii kuleta tija kwa maeneo yote.

Jambo lingine aliloliwekea mkazo ni mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya ambazo alisema zimeshamiri kijijini hapo Paje.

Kuhusu uvuvi, alisema atawawezesha wavuvi na kuweka kiwanda cha kusimika samaki ambapo Kijiji cha Paje shughuli zao kuu ni uvuvi hivyo kupata tija.



Kijana mchuuzi wa kashata akitumia mkusanyiko wa watu katika mkutano wa kampeni wa CCM, eneo la Paje, Mkoa wa Kusini Unguja jana, kama fursa ya kufanya biashara yake. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM yapeleka malalamiko ZEC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimewasilisha malalamiko yake mbele ya Kamati ya Maadili ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kutokana na matukio ya kushambuliwa na kupigwa kwa wafuasi wake wakiwa katika mikutano ya kampeni.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdalla Juma Sadalla, alisema hayo juzi Pemba alipowatembelea wafuasi wa chama hicho ambao walijeruhiwa kwa kushambuliwa kwa mawe na silaha za jadi na watu wanaodaiwa kuwa wafuasi wa ACT-Wazalendo.

Alisema matukio ya aina hiyo hayakubaliki kwa sababu lengo lake kubwa kuwatisha wafuasi wa CCM, ili washindwe kutumia haki yao ya kidemokrasia kupiga kura.

"Siasa za chuki na uhasama zimepitwa na wakati kwa sababu zitasababisha uvunjifu wa amani ya nchi na kuwatia taharuki wananchi kushindwa kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii," alisema.

"Chama Cha Mapinduzi tumeandika barua ya malalamiko kwa kamati ya maadili ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kuhusu matukio ya vitendo vinavyofanyika na wafuasi wa vyama vya siasa kwa kuwashambulia wafuasi wa CCM. Tumesikitishwa na matukio mawili yaliyojitokeza hivi karibuni," alisisitiza.

Naye Katibu wa Itikadi na Uenezi Mkoa wa Kusini Pemba, Abdalla Khamis, alisema wamesikitishwa na tabia iliyojitokeza sasa kwa wafuasi wa CCM kushambuliwa wakati wanaporudi katika mikutano ya kisiasa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**DEREVA NA MAUZO**, KATIKA KAMPUNI YA MAJI NAFASI 8 0767 – 269677.

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ALLEN ISSA KAIZA,** Anatangaza kupotelewa kwa result slip yenye index namba **S 3905-0005** kilichotolewa na shule ya UWATA SECONDARY mwaka 2019 yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/748903/2020**

115952102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ESTIM CONSTRUCTION CO. LTD**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA **KADI YA GARI** AINA YA **NISSAN PICK-UP**
YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 595 BRZ.** CHASSIS NAMBA **ADNCUD22Z0010105.**
ENGINE NAMBA **ZD30272709K.**
YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **DAR/MSI/RB/740528/2020.**

215951002

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na 79 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU GERNARD IDDI MSAMANGA**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**BERNADETTE JOSEPH MSAMANGA**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 mwezi 11 mwaka 2020.
Imewasilishwa Dar ES Salaam,leo tarehe 12 mwezi wa 10 mwaka 2020.

NAIBU MSAJILI

115950902

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY IN THE DODOMA OF DODOMA**
AT DODOMA
CIVIL CASE NO.13 OF 2020

**RAMADHANI KAIRO**...................................... PLAINTIFF (S)
VERSUS
**ASAM OIL CO. LTD**...................................... DEFENDANT(S)

SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE
( O.V.r I CPC)

**To ASAM OIL CO. LTD**
WHEREAS the above named plaintiff (s) has /have instated a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint.

YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty-one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the plaintiff if there are more defendants than one and the defence is not joint defence you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.

AND TAKE NOTICE that if you default in filing the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgement against you
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before

Hon...............
SENAPEE Judge/Magistrate on the 21 day of 10 2020 at 8:30 O'clock in the forenoon/afternoon
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COUTR this 19 day of 10, 2020.

215951502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
**MJINI-MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi **No;314/2020**
Ombi la **ERICK MICHAEL MSALANGE**
,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu
**RUTH MICHAEL KANYANGU.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **02/11/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **20/10/2020.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**DICKSON EMANUEL MNYUKWA** Anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.3418/0039** kilichotolewa mwaka 2019 na shule ya secondary MELI, yeyote atakayeiona atoa taarifa polisi. Polisi taarifa **DAR/MBA/RB/74769/2020**

115951302

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**MUSA JOHN MOGOTA,** Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3699-0051** kilichotolewa mwaka 2018 na shule ya secondary KIZUMBI yeyote atakayekiona atoa taarifa polisi.\ Polisi taarifa **9910819415011**

115951102


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Dola bilioni 2.4 zasakwa Sahel ya Kati

**SAHEL YA KATI,** BURKINA FASO

MATAIFA matatu yaliyo ukanda wa kati wa Sahel nchini Burkina Faso, ikiwamo Niger na Mali wanahitaji Dola bilioni 2.4, baada ya kukumbwa na janga kubwa la kibinadamu linalokabili wakazi wa maeneo hayo.

Jana, mjini Copenhagen nchini Denmark kulifanyika mkutano wa ngazi ya mawaziri wenye lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya suala hilo.

Takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya watu milioni 1.5 katika eneo hilo wamelazimika kukimbia makazi yao kutokana na ghasia, idadi ambayo ni mara 20 zaidi ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita.

Pia, ukatili wa kijinsia umeongezeka, mamilioni ya watoto hawako shuleni, huduma za msingi za afya na za kijamii hazipatikani.

Kwa sasa hali ya ukosefu wa chakula ni mara tatu zaidi ikilinganishwa na mwaka mmoja uliopita huku umaskini na mabadiliko ya tabianchi vikitishia mbinu za kawaida za watu kujipatia kipato na hivyo kufanya watu zaidi ya milioni 13 kuhitaji misaada ya kibinadamu.

Miongoni mwao hao ni watoto milioni saba, walioathiriwa na mapigano sambamba na janga la ugonjwa wa virusi vya corona au COVID-19.

Akifafanua kuhusu janga linalokumba wakazi wa Sahel ya Kati hususan Burkina Faso, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa, WFP, David Beasley alisema.

Akizungumzia mkutano huo wa kuchangia fedha, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres alisema, Sahel ya Kati iko katika msambaratiko na kunahitaji msaada wa kibinadamu. **UN**

# Wakimbizi wakimbia makazi nchini DRC

**KIVU KUSINI,** DRC

WATU kutoka jamii mbalimbali katika kijiji cha Mikenge Mkoa wa Kivu Kusini, Mashariki mwa DRC, wameendelea kulaumiana kila upande kuunga mkono makundi yenye silaha.

Kwenye Milima ya Minembwe, maelfu ya wakimbizi, waliokimbilia karibu na kambi za kikosi cha Umoja wa Mataifa nchini DRC, MONUSCO, na hawana msaada wa kimataifa.

**Ndio, ni watu kutoka hapa, kutoka kijiji hiki. Mvulana aliyepoteza maisha hapa, baba yake bado yuko hapa.**

Katika kijiji hiki cha Mikenge kuna karibu wakimbizi 3,000, hasa watu kutoka jamii ya Banyamulenge na kwamba walikumbwa na mashambulizi mengi.

Wakihojiwa na RFI, wakimbizi hao walisema walishambuliwa mara 20 na wanawajua waliotekeleza mashambulizi hayo.

Philemon Chiza, mmoja wa wawakilishi wao, alisimulia shambulio la hivi karibuni la Julai.

"Nitawaonyesha walikotokea. Wapiganaji wa kundi la Mai-Mai walitokea kwenye mlima huu, kwa njia hii. Waliingia kambini, wakafyatua risasi. MONUSCO ilijaribu kukabiliana nao, lakini askari kadhaa walijeruhiwa.

Hata hivyo Chiza alibaini kwamba anawajua wapiganaji hao wa kundi la Mai-Mai waliotekeleza shambulio hilo.

"Ndio, ni watu kutoka hapa, kutoka kijiji hiki. Mvulana aliyepoteza maisha hapa, baba yake bado yuko hapa." **RFI**



Dawa za kulevya aina ya cocaine zilizokuwa zimefichwa kwenye mabegi na nguo za ndani. Polisi nchini Ethiopia, inawashikilia raia wa kigeni 13 wa Nigeria na mmoja wa Brazil, baada ya kukamatwa kwenye uwanja wa ndege mjini Addis Ababa. **PICHA: ETHIOPIAN FEDERAL POLICE**

# Rais Trump amkosoa mtaalamu wake corona

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemkosoa vikali daktari mkuu wa magonjwa ya kuambukizwa Marekani, Anthony Fauci, kulingana na ripoti za vyombo vya habari nchini humo.

Taarifa hizo zinasema akiwa mbele ya wafanyakazi wa timu yake ya kampeni ya uchaguzi, Trump alimfananisha Fauci na "janga".

Trump pia alisema mtaalamu huyo angesikilizwa, basi idadi ya raia wa Marekani waliokufa kutokana na ugonjwa wa COVID-19 ingekuwa kubwa zaidi.

Trump na Fauci, ambaye ni mtaalamu katika kikosi chake cha kupambana na ugonjwa huo wamekuwa wakivutana juu ya namna ya kuudhibiti ugonjwa huo.

Virusi vya corona vimesababisha vifo vya watu 219,000 nchini Marekani, na kumpunguzia umaarufu kiongozi huyo wa Chama cha Republican. Fauci amekuwa akipendekeza hatua kali kuendelea kuzingatiwa dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona, hata hivyo Trump anampinga na kusisitiza kwamba maambukizi yameshapungua kasi Marekani.

Aidha, inaelezwa kuwa maambukizi ya corona yamefikia milioni 40 duniani.

Kulingana na Chuo Kikuu cha John Hopkins ambacho kinakusanya takwimu kutoka duniani, idadi hiyo ilifikia hapo juzi. Aidha, wataalamu walisema idadi halisi inaweza kuwa kubwa zaidi ya hiyo. Hadi sasa, zaidi ya watu milioni 1.1 wamefariki kutokana na virusi vya corona, ingawa wataalamu pia wanaamini idadi halisi inaweza kuwa kubwa zaidi ya hiyo.

Marekani, India na Brazil ndiyo mataifa yanayoripotiwa kuwa na idadi kubwa zaidi ulimwenguni kote.

Hata hivyo, ongezeko la kimataifa la maambukizi la wiki za hivi karibuni limekuwa likishuhudiwa zaidi barani Ulaya, ambako zaidi ya watu 240,000 wamefariki kutokana na janga hilo hadi sasa. **DW**

## Diallo ajitangazia ushindi kabla ya matokeo

**CONAKRY,** Guinea

KIONGOZI wa upinzani nchini Guinea, Cellou Dalein Diallo, amejitangaza mshindi katika uchaguzi wa urais uliofanyika mwishoni mwa wiki, kabla ya kutangazwa kwa matokeo rasmi.

Diallo aliwaambia wanahabari na wafuasi wake kwamba ameshinda duru ya kwanza ya uchaguzi.

Hakutoa takwimu zozote, lakini alisema kuwa hitimisho lake ni kutokana na hesabu ya chama chake wala sio tume rasmi ya uchaguzi.

Tume ya uchaguzi ilijibu kwa kusema shughuli ya kuhesabu kura bado inaendelea na hiyo ndio pekee yenye mamlaka ya kumtangaza mshindi.

Wafuasi wa Diallo ambao walikuwa wamekusanyika kusherehekea walitawanywa na maofisa wa polisi.

Baadaye aliandika ujumbe kwenye Twitter kwamba watu watatu wameuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa na polisi.

Raia wa Guinea wamekuwa wakiandamana kwa miezi kadhaa tangu Rais Alpha Condé, alipotangaza kuwania muhula wa tatu.

Matokeo ya uchaguzi huo uliotanda wasiwasi yanatarajiwa kutolewa leo na baada ya hapo wagombea watakuwa na siku nane za kukata rufani ikiwa wana malalamiko yoyote.

Mgombea wa urais anahitaji zaidi ya asilimia 50 ya kura kupata ushindi wa moja kwa moja au kutakuwa na duru ya pili ya uchaguzi mkuu, Novemba 24, mwaka huu. **BBC**

# PICKFORD AKWEPA RUNGU LA FA KWA VAN DIJK



**LONDON,** England

GOLIKIPA wa Everton, Jordan Pickford, hatakutana na rungu la FA kwa kumfanyia faulo mbaya mlinzi wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk katika mechi ya 'dabi' ya jiji moja, Jumamosi iliyopita.

Chama cha Soka England, FA kimelirudia tukio hilo kwa kuwaulizia waamuzi na wasimamizi wa VAR na kuamuliwa kwamba haikuwa faulo.

Beki huyo wa Liverpool alipata majeruhi ya goti ambayo yatamfanya kuwa nje kwa muda mrefu wa takriban miezi sita hadi minane.

Licha ya kurudia maamuzi ya waamuzi kwenye mchezo huo, FA ina mamlaka madogo ya kuamua tofauti na kile walichokiona waamuzi, ambapo baada ya kutazama wamebaini kuwa ilikuwa ni sehemu ya changamoto ya kimichezo.

# Klopp: Everton itanitoa jasho EPL msimu huu

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, anaweza kuwa mshindani mkuu wa Liverpool katika Ligi Kuu ya England, kwa mujibu wa Jurgen Klopp.

Everton inaongoza katika jedwali la ligi ikiwa imeshinda mara nne katika mechi tano chini ya usimamizi wa raia huyo wa Italia ambaye aliajiriwa Desemba iliyopita.

Na katika mchezo wao Jumamosi, Everton na Liverpool zilitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na hivyo wao kuendelea kuongoza msimamo wa ligi, huku kikosi cha Klopp kikiwa nafasi ya tatu.

"Kile ninachofikiria kuhusu Carlo Ancelloti hakikuwa siri. Ni mtu mzuri," alisema Klopp akiiambia BBC.

"Niliposikia kwamba atakuwa kocha mpya wa Everton, nilijua ushindani mkali mwingine umewasili Uingereza.

"Walifanya biashara nzuri ya kununua wachezaji wakati wa dirisha la uhamisho la msimu uliopita. Walipata wachezaji waliowahitaji kuimarisha kikosi ambacho tayari kilikua kizuri.

"Pamoja sasa ni kuzoea kile ambacho anataka kuwafanya kuwa bora zaidi."

Ancelloti alimrithi Marco Silva kama kocha wa Everton, baada ya kushinda mataji ya ligi akiwa Italia, Ujerumani, Ufaransa na England akiifundisha Chelsea msimu wa 2009-10.

Pia ameshinda mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.





# 'Madrid haikutakiwa kumwachia Ronaldo'

**MADRID,** Hispania

CRISTIANO Ronaldo ni "mashine ya kujitolea" ambaye kamwe hakutakiwa kuruhusiwa kuondoka Real Madrid, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Shakhtar Donetsk, Luis Castro.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or alifunga mabao 450 kwa Madrid na kushinda mataji 15 kwa kipindi cha miaka tisa aliyokaa kwa miamba hao wa soka la Hispania.

Aliondoka na kwenda Juventus kwa fedha ndefu Julai mwaka 2018 na ameendelea kuwa na kiwango cha kuvutia akiwa amefunga mabao 68 katika mashindano yote, akiisaidia timu hiyo kutwaa taji la Serie A.

Kuelekea mchezo wa Shakhtar wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa Kundi B dhidi ya Madrid leo Jumatano, Castro amehoji uamuzi wa mabingwa hao wa LaLiga kumwachia nyota huyo aondoke.

"Wakati ukiwa na Cristiano kwenye timu yako hutakiwi kumwachia aondoke. Kamwe," alisema akinukuliwa na Marca.

"Tunamzungumzia mchezaji bora, mchezaji ambaye ni kama mashine na mwenye uwezo wa kujitolea kwa ajili ya timu.

"Kwa uhakika kabisa, Ronaldo hakupaswa kuachiwa aondoke Madrid na sasa wanamkosa mtu wa kuwapa matokeo kwenye mchezo muhimu. Lilikuwa kosa kubwa, ambalo kamwe mimi nisingeweza kulifanya."

# Arteta apewa darasa la kuepuka vipigo Arsenal

**LONDON,** England

NAHODHA wa zamani wa Arsenal, Tony Adams, amemtaka Mikel Arteta kurudi katika mfumo wa kutumia mabeki wanne baada ya timu hiyo kuchapwa bao 1-0 na Manchester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumamosi iliyopita.

Arteta aliamua kutumia mfumo wa mabeki watatu wa kati na mawinga wawili, licha ya kwamba mfumo huo uliifanya timu kukosa ujuzi kwenye robo ya tatu ya uwanjani, ambapo ni eneo la kushambulia.

Na kitendo hicho cha kutumia mabeki watatu wa kati kiliwafanya Arsenal kupoteza mechi yake ya pili msimu huu jambo linalomfanya beki wa zamani wa miamba hiyo, Adams kumwambia Arteta abadilike na atumie safu ya mabeki wanne.

"Nadhani huu ni wakati wa kutumia mabeki wanne. Nimekuwa nikisema hili tangu mwanzo wa msimu," alisema akinukuliwa na Sky Sports.

Adam alisema ili Arsenal iwe na nguvu zaidi kwenye safu yake ya ulinzi ni lazima ihakikishe inakuwa na mabeki wanne kwa ajili ya kupunguza mashambulizi, huku akiwatumia viungo wawili.

"Nadhani atabadilika kwenye mchezo ujao, kwa sababu hilo hata yeye atakuwa ameliona, walinzi watatu nyuma ni mfumo mbaya ukikutana na timu inayoshambulia zaidi kama ilivyotokea kwa Manchester City."






# AZPILICUETA SASA AMTETEA KEPA

**LONDON,** England

NAHODHA wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, amesisitiza "hana shaka" na golikipa, Kepa Arrizabalaga kwamba atarudi kwenye kiwango chake.

Baada ya makosa kadhaa ya Kepa, Chelsea ilimsajili Edouard Mendy kutoka Rennes Septemba, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal aliumia nyama za paja mapema mwezi huu.

Kepa alirudi kwenye kikosi cha kwanza dhidi ya Southampton, Jumamosi, lakini alifanya tena kosa wakati Chelsea wakitoka sare ya mabao 3-3.

Lakini kabla ya mchezo wa jana wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Sevilla, Azpilicueta amesema Kepa anaweza kubadilika.

"Kwenye soka tunakuwa na wakati mgumu. Kwa nafasi yangu kama nahodha, namjua Kepa, tena kwa muda mrefu, mara zote najaribu kumsaidia yeye," alisema beki huyo akiwaambia waandishi wa habari.

"Na ni kweli kwamba, ni wakati mgumu kwake kwa sasa, maana kila mmoja anamwona kama mwenye kuigharimu timu, lakini naamini atarudi kwenye kiwango chake na kusahihisha makosa yake.

"Anatakiwa kupewa sapoti kwa sasa ili aweze kujiona ni mtu muhimu kwenye kundi letu na hivyo ndivyo ninavyofanya kama nahodha."

# *Ibrahimovic zaidi ya Ronaldo Serie A*

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic ana mchango mkubwa zaidi kwa soka la Italia kuliko Cristiano Ronaldo, kwa mujibu wa kocha wa zamani wa AC Milan na Juventus, Alberto Zaccheroni.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, amekuwa na kiwango cha kuvutia na kutoa mchango mkubwa tangu alipojiunga tena na Milan Januari, akifunga mabao 11 katika mechi 20 katika nusu ya pili ya msimu wa 2019-20.

Pia amekuwa na kiwango cha kuvutia msimu huu licha ya kuwa nje ya dimba kwa mwezi mmoja kutokana na kupatikana na maambukizi ya virusi vya corona.

Tangu kuanza kwa msimu huu amefunga mabao manne katika mechi mbili tu za ligi na alifunga mara mbili wakati Milan ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Inter, Jumamosi iliyopita.

Ronaldo alijiunga na Juve kutoka Real Madrid mwaka 2018 na amefunga mabao 68 katika mechi 91 alizocheza kwenye mashindano yote.

Zaccheroni sasa hana shaka kwamba, Ibrahimovic ndiye mwenye mchango mkubwa zaidi katika Ligi ya Serie A.

"Nimewanoa mabingwa wakati nikiwa kocha, kutoka (Oliver) Bierhoff hadi (George) Weah na Adriano, lakini najutia sikuwahi kumnoa Ibrahimovic," alisema akiiambia Il Giornale.

"Yeye ni mchezaji wa daraja la juu kabisa, na sielewi kwa nini hajawahi kushinda tuzo ya Ballon d'Or.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UPAMECANO ATAJWA MRITHI VAN DIJK LIVER

●●● Hakuna namna yoyote lazima Liverpool isajili mlinzi wa kati Januari na si mwingine bali...

**LUVERPOOL,** England

JAMIE Carragher ameitaka Liverpool kufanya vyovyote inavyoweza kumsajili mlinzi wa RB Leipzig, Dayot Upamecano Januari baada ya kumpoteza Virgil van Dijk aliyeumia goti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alilazimika kutolewa nje mapema wakati 'Wekundu' hao wakilazimishwa sare ya kufungana mabao 2-2 na Everton, Jumamosi iliyopita baada ya kugongana na kipa, Jordan Pickford.

**Majeraha hayo ya Van Dijk yatamweka nje kwa kipindi kirefu cha msimu huu.**

Awali Liverpool ilihusishwa kumtaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, Upamecano na sasa Carragher ameitaka klabu hiyo kukamilisha usajili huo katika dirisha la Januari.

"Usajili ujao wa Liverpool unahitaji mlinzi wa kati na kwa vyovyote, Jurgen Klopp lazima amsajili Upamecano," alisema Carragher akiiambia Sky Sports.

"Dejan Lovren ameondoka na hawakutafuta mrithi wake na wana mabeki wa kati watatu na mmoja wao ni Joel Matip, ambaye mara zote ameumia.

"Kuna swali sasa kuhusu Joe Gomez. Hakuna namna yoyote lazima Liverpool isajili mlinzi wa kati Januari na si mwingine bali Upamecano."

## ZISIKUPITE

### SON KUONGEZWA MSHAHARA

KLABU ya Tottenham Hotspur wanajiandaa kumuongezea Son Heung-min mshahara hadi pauni 150,000 kwa wiki ili kumshawishi mshambuliaji huyo raia wa Korea Kusini mwenye umri wa miaka 28, akubali kusaini mkataba mpya. ***(Mail)***

### HAALAND AITAKA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, mwenye umri wa miaka 20, angependa kwenda Real Madrid kuliko Manchester United. ***(ABC via Manchester Evening News)***

### DEMBELE, BRAITHWAITE SOKONI

BARCELONA wanataka kumruhusu mshambuliaji wake, Ousmane Dembele, mwenye umri wa miaka 23 na Martin Braithwaite mwenye miaka 29, kuondoka ili kutoa fursa kwa Memphis Depay kutoka Lyon mwenye miaka 29, na Myron mwenye miaka 19 kutoka AZ Alkmaar ***(Todofichajes)***

### INGS KUIZIMA TOTTENHAM

MSHAMBULIAJI wa Southampton na England, Danny Ings, mwenye umri wa miaka 28, anakaribia kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, huku Tottenham wakimwania.***(Athletic)***

### WHITE AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanamtaka mlinzi wa Brighton, Ben White, mwenye umri wa miaka 23, baada ya Leeds United kushindwa kumsajili kipindi cha dirisha la usajili. ***(Football Insider)***

### SARRI ANUKIA FIORENTINA

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, anakaribia kupata dili la kuinoa klabu ya Fiorentina iwapo wataamua kumfukuza kocha wao wa sasa, Giuseppe. ***(Calcio Mercato)***

### ZABALETA KURUDI MAN CITY

KLABU ya Manchester City ipo tayari kumpokea, Pablo Zabaleta anayerejea katika klabu hiyo kuchukua wadhifa wa uongozi, baada ya kustaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 35 wiki iliyopita. ***(Mail)***

### DYBALA KUSAINI MKATABA

JUVENTUS wana imani kuwa mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala, mwenye umri wa miaka 26, atasaini mkataba mpya. ***(Tuttosport)***

### JONES KUONDOKA UNITED

MLINZI wa Manchester United, Phil Jones, mwenye umri wa miaka 28, anataka kuondoka katika klabu hiyo wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Sun)***

### WIJNALDUM, LIVER KUACHANA

KIUNGO wa kati wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum, 29, anaweza kujiunga na Barcelona wakati wa dirisha la usajili la Januari. Mchezaji huyo kwa sasa yuko mwaka wa mwisho wa mkataba wake na msimu ujao atakuwa huru. ***(AD, via Sky Sports)***

### PSG KUMSAJILI ERIKSEN

KLABU ya Paris St-Germain itajaribu kumsajili nyota wa Inter Milan, Christian Eriksen, 28, kwa euro milioni 20, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark akihangaika kupata nafasi kule Serie A. ***(Todofichajes)***

# HABARI MICHEZO

## Chaneta yatangaza kambi Ligi Muungano

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), umezitaka timu zote ambazo zinajiandaa na mashindano ya Ligi ya Muungano yatakayofanyika kuanzia Novemba 28 hadi Desemba 7, mwaka huu jijini Tanga, kuripoti kambini kuanzia Novemba 26.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chaneta, Devota Marwa, alisema kwa upande wa Tanzania Bara timu zote zinaendelea vizuri na mazoezi.

Alisema maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri na kuomba wadau mbalimbali kujitokeza kuwaunga mkono.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kila timu inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kwenda kufanya vizuri siku ya mashindano," alisema Devota.

Alisema kwa upande wa timu za visiwani Zanzibar, wamefanya nao mawasiliano na kujuzwa kwamba timu zinaendelea kujinoa kuelekea mashindano hayo ambayo yanatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa.

"Tunaomba wachezaji wote ambao wanajiandaa na mashindano hayo waongeze juhudi ya kufanya mazoezi ili waweze kufanya vizuri," alisema.

Mashindano hayo yatashirikisha jumla ya timu 12 kutoka Tanzania Bara pamoja na Visiwani.

## Mabondia wa Tanzania kupanda ulingoni Latvia

**Na Adam Nyangasa,** TUDARCo

BAADA ya anga kimichezo kufunguka katika nchi mbalimbali duniani, Katibu wa Chama cha Ngumi za Kulipwa Tanzania (PST), Anthony Rutagamba maarufu Ruta, amesema kwa sasa mabondia wao watatu wanaendela kujiandaa na mapambano yao yatakayofanyika Oktoba 31, mwaka huu nchini Latvia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ruta aliwataja mabondia hao watakoiwakilisha Tanzania kuwa ni Happy Mwigike, Flora Machela na Nasibu Ramadhan.

Alisema mapambano hayo si ya kugombania ubingwa na kwamba Flora atazichapa na Jekatarina Marcenko kwenye pambano la raundi nne wakati Happy yeye atazipiga na Elvina White pambano la raundi nne huku Ramadhan yeye akiwa na shughuli pevu ya raundi sita dhidi ya Artjoms Ramlavs.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kufungua mipaka na safari za nje, mabondia wetu wapo vizuri na wanaendelea na maandalizi kuelekea mapambano yao, ningependa tu kuwaomba Watanzania waendelee kusapoti mchezo huu," alisema Ruta.

Kwa upande wa Happy ambaye ni miongoni mwa mabondia watakaopanda ulingoni siku hiyo, alisema yuko 'fiti' na bado anaendelea na maandalizi kuelekea pambano hilo.

# BARAZA ATOA SABABU KICHAPO KWA COASTAL

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, ameeleza kushangazwa na uzito wa wachezaji wake kuonekana kama wamebeba mabegi mgongoni kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union hali iliyowasababishia kipigo cha mabao 3-0 juzi kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

**Baraza ambaye ni raia wa Kenya, alisema hajui nini kimetokea, na kuongeza kuwa hajawahi kufungwa idadi hiyo ya mabao kwa timu za kawaida zaidi ya Simba tu.**

"Yalikuwa ni makosa yetu wenyewe, tuliwapa nafasi kubwa ya kutawala mechi, viungo walikatika, halafu wachezaji wangu walikuwa wazito. Sijui nini kilitokea, lakini walikuwa kama wamebeba mabegi mgongoni. Ni Simba tu iliyowahi kutufunga mabao manne kutokana na uwezo wao, lakini sijawahi kufungwa idadi hii ya mabao na timu zingine, tena kwa makosa yetu wenyewe, lakini hili nitalifanyia kazi," alisema kocha huyo.

Kwa upande wa kocha wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema kushinda mabao 3-0 juzi si kama timu imeimarika sana, ila wametumia nafasi ambazo awali zilikuwa zinapatikana, lakini hazitumiwi vizuri.

"Nilisema huko nyuma kuwa timu yangu inatengeneza nafasi nyingi, lakini hatuzitumii, ila jana tumerekebisha makosa na tumetumia nafasi zilizopatikana, hilo ndilo lililotokea," alisema Mgunda.

Kocha huyo ameisifu Biashara kuwa ni timu nzuri na kilichowakuta ni mambo ya mchezo wa soka ambayo wakati mwingine huwa na matokeo ya kikatili.

Kwa matokeo hayo, timu hizo zote zinakuwa zimecheza mechi saba, Coastal Union ikifikisha pointi nane, huku Biashara United ikibakia na pointi 13 na kushindwa kuzipiku Simba na Yanga ambazo pia zina pointi hizo, kesho zikishuka viwanja tofauti kucheza mechi zao za sita.

Simba itakuwa ugenini, Uwanja wa Nelson Mandela dhidi ya Prisons, huku Yanga ikiwa nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Polisi Tanzania.




Kocha wa KMC FC, Habibu Kondo, akitoa maelekezo kwa wachezaji wake wakati wa mazoezi yaliyofanyika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, wakijiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting iliyopigwa jana katika Uwanja wa Mabatini, Pwani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Novatus alia umakini sare Polisi Tanzania*

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Gwambina FC, limesema wachezaji wake walipoteza umakini katika mchezo uliopita dhidi ya Polisi Tanzania, ambao ulichezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha na kumalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka jijini Arusha, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Fulgence Novatus, alisema wachezaji wake walipata nafasi nyingi za wazi lakini walishindwa kuzitumia.

Alisema hajaridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake, kwa kuwa walistahili kushinda kwa mabao mengi, lakini kukosa umakini kukawasababishia sare hiyo.

"Wachezaji wangu walishambulia sana, isipokuwa walipoteza umakini ambao umetusababishia kuondoka na pointi moja," alisema Fulgence.

Alisema baada ya mchezo kumalizika alikaa na kuzungumza na wachezaji kama sehemu ya kuanza kufanyia kazi makosa aliyoyaona.

Kocha huyo alisema kwa sasa wachezaji wote wanaendelea vizuri isipokuwa Paul Nonga ambaye ni majeruhi wa muda mrefu na kwamba jana walipumzika kabla ya leo asubuhi kuanza safari ya kuelekea jijini Tanga tayari kwa mechi yao inayofuata Oktoba 24 dhidi ya Coastal Union .

Novatus alisema baada ya kufanya makosa katika mechi iliyopita na kujikuta wakiambualia pointi moja, lengo lao sasa ni kuvuna alama zote tatu watakapoikabili Coastal kwenye mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Mkwakwani.

# Michezo

Jumatano Oktoba 21, 2020

Nipashe




Upamecano atajwa mrithi Van Dijk Liver UKURASA 22

USIKU WA ULAYA...



Wachezaji wa Liverpool wakijifua chini ya kocha wao, Jurgen Klopp (aliyevaa kofia), tayari kwa kuivaa Ajax kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakayopigwa Amsterdam, Uholanzi leo. **PICHA: MTANDAO**

# Simba, Yanga sasa kusubiri kwa Azam

## ●●● Yazidi kuzikimbiza ikijiwekea rekodi yake Ligi Kuu Bara, watani hao wa jadi kujiuliza kesho kwa...

**Na Adam Fungamwango**

MOTO unaoendelea kuwashwa na Azam FC kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara, ni wazi sasa mabingwa watetezi, Simba pamoja na watani zao, Yanga watalazimika kusubiria kuona timu hiyo ikipoteza huku wao wakishinda mechi zao ili kuweza kuishusha kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu.

**Azam jana ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ihefu FC katika mechi ya ligi hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.**

Ushindi huo ni wa saba mfululizo msimu huu, hiyo ikiwa ni rekodi mpya kwa klabu hiyo tangu imepanda Ligi Kuu msimu wa 2008/09 kwani haijawahi kushinda mechi za ligi mfululizo kwa idadi hiyo.

Matokeo hayo yanaifanya Azam kufikisha pointi 21, nane mbele ya Simba na Yanga ambazo zipo michezo miwili nyuma kila moja, lakini hata kama zitashinda mechi hizo bado zitakuwa nyuma kwa alama moja dhidi ya vinara hao.

Katika mechi hiyo ambayo Ihefu FC ilikuwa chini ya Kocha mpya, Zuberi Katwila, aliyekabidhiwa jukumu hilo Jumapili usiku baada ya kubwaga manyanga Mtibwa Sugar, shukrani hazina budi kumwendea straika hatari wa Azam, Prince Dube ambaye jana hakufunga bao hata moja, lakini alitoa pasi zote mbili za mwisho zilizozaa mabao hayo.

Akiwa kwenye wingi ya kushoto, alipiga majalo safi iliyomkuta Ayoub Lyanga na kuujaza wavuni kwa kichwa dakika ya 55, huku akimwacha kipa Andrew Kayuni akiwa hana la kufanya.

Dakika ya 83, Dube tena aliambaa na mpira kwenye wingi ya kulia na kumimina krosi safi iliyounganishwa nyavuni kwa kichwa na Iddi Nado aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya mfungaji wa bao la kwanza, Lyanga.

Dube ambaye hadi sasa yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji vinara wa Ligi Kuu akiwa na mabao sita, amekuwa chachu ya ushindi kwa Azam msimu huu, lakini hadi sasa kati ya mabao hayo ni moja tu ndilo amefunga wakiwa ugenini wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga mengine yote alitupia wakiwa nyumbani kwenye dimba la Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

Kwa kasi ya hii ya Azam ya kushinda, ni wazi sasa njia pekee ya Simba na Yanga kuishika ni kuendelea kushinda mechi zao na timu hizo kuhakikisha zitakapokutana na 'Wanalambalamba' hao, zinaondoka na pointi zote tatu.

Kutokana na matokeo hayo ya jana Ihefu sasa imebaki na pointi zake tatu, ikicheza mechi saba, kushinda moja na kufungwa sita.

Katika mechi ya jana, Azam ilitawala mechi na kukosa mabao mengi kupitia kwa Dube na Obrey Chirwa, huku nafasi pekee kwa Ihefu ilipatikana kupitia kwa Emmanuel Kichiba aliyepiga kona iliyokwenda moja kwa moja na kugonga mwamba wa juu na kudundia nje ya mstari dakika ya 35 kipindi cha kwanza.

Simba na Yanga zitashuka dimbani kesho kujaribu kupunguza wigo huo wa pointi kutoka kwa Azam FC kwa kuzivaa Tanzania Prisons na Polisi Tanzania katika mechi zitakazopigwa Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga na Uhuru jijini Dar es Salaam.

# Sven amaliza kazi Simba kwa Prisons

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya kuwataka wachezaji wake kuwa makini katika mchezo wao wa kesho dhidi ya Tanzania Prisons kutokana na kupata ugumu wanapocheza ugenini, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck (pichani), ameweka wazi kuwa tayari amewapa mbinu nyota hao na kwamba matokeo mazuri yapo mikononi mwao.

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya mazoezi ya timu hiyo, Sven alisema mchezo huo hautakuwa mwepesi kutokana na ugumu wanaoupata wakiwa viwanja vya ugenini.

"Nimewaona wapinzani wetu, mchezo wao ni wa nguvu, hautakuwa mwepesi kwetu, tunapaswa kuwa na mbinu nyingi kuweza kupata matokeo mazuri," alisema Sven.



Alisema tayari amewapa maarifa ya namna ya kucheza na wapinzani wao hao na si kwa kucheza soka walilolizoea.

"Matokeo mazuri kwetu wanayo wachezaji, wakifuata vizuri kile ambacho tumewaelekeza na tutakachowaelekeza siku ya mchezo, basi tutakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata ushindi," aliongeza kusema Sven.

Aidha, kwa upande wake meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu alisema mpaka kufikia jana kikosi cha timu hiyo kilikuwa kwenye hali nzuri na kila mchezaji alikuwa fiti.

"Tumefanya mazoezi Mbeya jana (juzi) na leo pia (jana), tunashukuru hatuna majeruhi wapya, na sasa hivi (saa nane mchana jana) tupo njiani tunaelekea Sumbawanga," alisema Rweyemamu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >